**WANUSA** harufu ufisadi ujenzi uzio wa mnada

UKURASA 16



**KINANA:** Rais Samia msikivu, nchi imetulia

UKURASA 18




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Julai 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581381

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Uhalifu watoto wa kiume tishio jipya

**USHUHUDA** mahabusu ya watoto waibua ya kutisha... *Endelea ukurasa wa 3*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea tuzo kwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camilius Wambura, kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutambua na kuthamini mchango wa askari wa kike na kuwaamini kushika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye ufunguzi wa kongamano la Shirikisho la Kimataifa la Polisi Wanawake Kanda ya Afrika lililofanyika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**



Mgeni Rasmi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2022, Balozi Ombeni Sefue (kushoto), akikabidhi tuzo ya Mshindi wa Jumla kwa Mhariri Msanifu wa Gazeti la Nipashe, Sanula Athanas, katika hafla iliyofanyika mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ipp Media yatoa tena Mshindi wa Jumla katika tuzo za EJAT

UKURASA 2

UKURASA WA 9

## SERIKALI KUJENGA KITUO KIKUBWA CHA WARAIBU DAWA ZA KULEVYA

SERIKALI ina mpango wa kujenga kituo kikubwa cha huduma za utengamao kwa waraibu jijini Dodoma ili waweze kupata mafunzo ya ujasiriamali katika mwaka wa fedha...

## CHADEMA yatoa msimamo mkali zuio mikutano

UKURASA 18

UKURASA WA 19

## WATU 16 WAUAWA DARFUR SHAMBULIO LA ROKETI



CHAMA cha Wanasheria Mkoa wa Darfur kimesema watu 16 wameuawa kwa shambulizi la roketi ambalo limepiga nyumba za wakazi katika mkoa huo, magharibi mwa Sudan wakati wa majibizano ya roketi kati ya jeshi na wanamgambo wa msaada wa haraka (RSF)...

**MICHEZO** GAMONDI ATOA UCHAMBUZI WA KIKOSI YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA

# Tishio ongezeko makosa uhalifu watoto wa kiume

Na Restuta James

ULAWITI, unyang'anyi wa kutumia silaha, mauaji, wizi na matusi ni makosa yanayofanywa na watoto hasa wa kiume, mamlaka zimethibitisha.

Aidha, asilimia kubwa ya watoto wa kiume wanaofikishwa katika Mahakama ya Watoto jijini Dar es Salaam, wanashtakiwa kwa makosa ya ulawiti.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Meneja wa Mahabusu ya Watoto iliyopo Upanga, jijini Dar es Salaam, Darius Kalijongo, alisema aina hiyo ya uhalifu kwa watoto inachangiwa na malezi duni, makundi rika pamoja na umaskini kwa kipato cha familia.

Alisema watoto wanaotuhumiwa kwa makosa wamethibitika kuyatenda kweli.

Alitoa mfano kwamba katika kipindi cha miaka minne iliyopita (2018/2019-2021), jumla ya watoto wa kiume 448 walipokewa katika mahabusu hiyo, 150 kati yao walikuwa wamefanya unyang'anyi kwa kutumia silaha na 84 walilawiti wenzao.

Kalijongo alitaja makosa mengine yaliyofanywa na watoto wa kiume na idadi yao kwenye mabano kuwa ni mauaji (10), wizi (76), matusi (4), kujeruhi (6) na kuingia nchini bila kibali (36).

Kwa upande wa watoto wa kike, meneja huyo alisema waliofikishwa katika mahabusu hiyo kwa kipindi hicho ni 17 ambao walikuwa wanakabiliwa na makosa ya mauaji (5), kujeruhi (3), bangi (1) na kuingia nchini bila kibali (8).

Alisema vitendo vya ulawiti vinachangiwa na utandawazi, kwa watoto kuona kwenye televisheni au kwenye simu.

Alisema changamoto inayoikabili jamii kwa sasa ni wazazi pamoja na walezi kushindwa kutoa ushirikiano wakati wa mchakato wa marekebisho ya tabia, pale mtoto anapokuwa ametenda kosa.

Alitoa mfano kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022, mahabusu hiyo ilipokea watoto 123, kati yao 48 walikuwa wamefanya uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia silaha.

Makosa mengine na idadi ya watoto waliotenda kwenye mabano ni mauaji (4), wizi (25), ulawiti (6), ubakaji (11), kujeruhi (4) na uhujumu uchumi (1).

Makosa mengine kwa mujibu wa meneja huyo ni kuvunja na kuiba (2), kuingiza mifugo shambani (2), kupanga njama ya wizi (6), shambulio la aibu (1), kukutwa na mali ya wizi (1), kuingia nchini bila kibali (12) na kwamba hakuna aliyeshtakiwa kwa kukutwa na bangi wala kuua kwa kutokusudia.

"Changamoto kubwa zinazotukabili kwa sasa ni kuongezeka kwa makosa makubwa ambayo watoto wanashtakiwa nayo, mashauri ya mauaji (PI), kuchukua muda mrefu na kukosekana kwa programu endelevu ya ufuatiliaji hasa kesi inapokwisha," alisema.

Alisema kwa Jiji la Dar es Salaam, maeneo ambayo watoto wanatoka ni Bunju, Temeke, Mbagala, Kigamboni, Chanika, Kinyerezi, Bagamoyo, Chalinze, Gongo la Mboto, Kigogo Luhanga, Kibaha, Mburahati, Tandika, Manzese, Mbezi Mwisho na Mbezi Juu.

Alisema kwa wanaoingia nchini bila kibali wanatoka nchi za Kongo na Burundi.

**MAHAKAMA YA WATOTO**

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Watoto iliyopo katika Kituo Jumuishi cha Temeke, Orupa Mtae, aliiambia Nipashe kwamba wanapokea kesi za madai na za jinai, zikiwamo za wizi, ubakaji na ulawiti.

"Kwenye makosa ya jinai, asilimia kubwa ya kesi tunazopokea hivi sasa ni za ukatili wa kingono na kijinsia. Kwa sasa nyingi ni za kulawiti kwa maana ya mtoto kumwingilia mwingine kinyume cha maumbile," alisema.

Alisema: "Takwimu halisi siwezi kukupa, lakini kesi za ulawiti ni nyingi sana ukilinganisha na hizi nyingine kama wizi, mengi tunayoyapokea ni ulawiti na kubaka; asilimia kubwa ni ulawiti."

Hakimu Orupa aliongeza: "Makosa ya kubaka yapo, lakini yanayoongoza ni kulawiti. Asilimia kubwa ni watoto wa kiume kuingilia wenzao wa kiume, chache sana za watoto wa kike kuingiliwa kinyume na maumbile."

Alisema tathmini yake imebaini kwamba watoto wanaojihusisha na makosa hayo kutokana na malezi duni ya wazazi au walezi.

"Natoa rai kwa wazazi kuwa macho zaidi katika malezi, wazazi pia wawajengee uwezo watoto wa kujitambua na kujikinga dhidi ya matendo haya," alisema.

Hakimu Orupa alisema watoto wengi wanashawishiwa na kurubuniwa kwanza kabla ya kufanyiwa vitendo hivyo na kueleza kuwa mzazi makini anaweza kumsaidia mtoto kabla ya kulawitiwa.

"Yule anayemfanyia tukio (ulawiti), haanzi moja kwa moja bali kuna vishawishi watoto wanafanyiana, kuna wengine wanasema walikuwa wanaangalia picha za ngono na kuambiwa afanye kama alivyoona, wengine wanajifunza kwa wenzao shuleni, kwa hiyo kabla ya tukio lenyewe, kuna vitu vya awali vinafanyika," alisema Orupa.

Hakimu Orupa alisema baadhi ya watoto wanajifunza na kufanya uhalifu kutokana na wazazi na walezi wao kutowalea ipasavyo kutokana na majukumu ya kutafuta kipato.

Alisema wazazi na walezi wengi, wanaondoka nyumbani alfajiri wakati ambao watoto nao wanajiandaa kwenda shule, na wanarudi wakiwa wamechoka kiasi cha kushindwa kuongea na watoto.

Hakimu huyo anawashauri wazazi kuweka utaratibu wa kuzungumza na watoto kila siku. "Inawezekana siku unayoongea naye ndiyo siku ambayo ameanza kushawishiwa, ukiongea naye utazuia tukio la ulawiti au ubakaji," alisema.

**MIPANGO YA BAADAYE**

Meneja wa mahabusu hiyo alisema wanakusudia kuanzisha programu endelevu zitakazowezesha watoto kujifunza stadi za maisha ikiwamo uchoraji, ufugaji wa kuku na samaki.

Alisema wanaimarisha eneo hilo kwa kutoa ujuzi wa ufundi, kilimo na ufugaji ikiwamo ushonaji, ususi, kilimo cha bustani, kompyuta na ufundi wa aina mbalimbali.

Alisema baadhi ya watoto wamepewa mitaji na vitendea kazi.

"Watoto watatu wamepewa vyerehani na sasa wanaendelea na shughuli za ushonaji, wanne wamewezeshwa kuanzisha biashara ndogondogo, wawili wanashiriki katika shughuli za kilimo na mmoja amejiunga na Chuo cha Uchungaji," alisema Kalijongo.

Aliongeza kuwa: "Watoto watano wameajiriwa na wengine wamejiajiri wenyewe na wanne wamerudi shule baada ya kesi zao kumalizika."

Alisema programu ya uchepushaji na kudhaminiwa na kuimarika kwa ushirikiano kati ya mahabusu hiyo na maofisa ustawi wa jamii, polisi na mahakama, kumepunguza idadi ya watoto katika mahabusu hiyo.

Ripoti za mamlaka hizo mbili zinakuja takribani miezi miwili tangu Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT), ianze utafiti na mapitio ya sheria zinazosimamia makosa dhidi ya maadili nchini.

Mei 12, mwaka huu, LRCT iliwakutanisha wakuu wa upelelezi wa jinai Tanzania Bara na Zanzibar na waendesha mashtaka wa mikoa ya Tanzania bara ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Bunge na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuiagiza Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya utafiti huo kutokana na ongezeko la vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini.

Kikao hicho kilichohudhuriwa na Katibu Mtendaji wa LRCT, Griffin Mwakapeje, kililenga kupata taarifa na takwimu za makosa hayo nchini na changamoto za kisheria wanazokabiliana nazo katika ukamataji, upelelezi na uendeshaji wa mashauri hayo mahakamani.

Makosa dhidi ya maadili ni pamoja na kubaka, genge la ubakaji, kujaribu kubaka, kuteka, udhalilishaji wa kingono, kuwaingilia kingono watu wenye ugonjwa wa afya ya akili, kumwingilia mtu asiye mke mwenye umri chini ya miaka 18 bila ridhaa yake na kuwatweza watoto kingono.

Makosa mengine ni udhalilishaji mkubwa wa kingono, uwakala wa ukahaba, kumiliki madanguro, kuingilia kinyume na maumbile (ushoga), kuzini na maharimu, kusambaza picha za ngono, ponografia kwa watoto na kwa njia ya mtandao na usagaji.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitula, alisema asilimia 40 ya mashtaka katika Wilaya ya Kigamboni ni ya mmomonyoko wa maadili, yakihusisha vitendo vya ulawiti na ubakaji.

Alisema kumekuwa na ongezeko la makosa ya ulawiti, ubakaji na ukatili wa kijinsia nchini.

"Makosa haya yapo nchi nzima, japo kuna mikoa na sehemu chache yanaonekana yapo zaidi, lakini ni tatizo kubwa kwa taifa letu...katika Wilaya ya Kigamboni mashtaka ambayo yapo mahakamani karibu asilimia 40 ni ya namna hii, kwa hiyo mnaweza kuona namna ambavyo tatizo ni kubwa," alisema.

Taarifa ya DPP iliungwa mkono na Hakimu Orupa aliyesema kesi nyingi za ulawiti wanazopokea katika mahakama yake zinatoka Wilaya ya Kigamboni.


**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya RUNGWE**
**Kituo cha TUKUYU MJINI...MKOA...MBEYA**

**Shauri la Mirathi No. 18/2016**

**WASIMAMIZI WA MIRATHI: ANNA SANGA NA MOSHI HASSAN**

**MSIMAMIZI NO. 2: MOSHI HASSAN**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Unaamriwa ufike katika Mahakama ya Mwanzo Tukuyu Mjini tarehe 22/8/2023 kuja kujibu kwanini hamjawasilisha hesabu za mirathi tangu mwaka 2016 mlipoteuliwa, na kwanini msiondolewe kwenye usimamizi wa mirathi.

**Angalia:** Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, na ikathibitika kuwa ulipokea wito huu, basi Mahakama inaweza ikasikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo na ikatoa maamuzi ambayo yatakuhusisha na wewe.

Hati hii imetolewa leo tarehe 17/7/2023 imesainiwa kwa mkono wangu na kugongwa muhuri wa Mahakama.

PRIMARY COURT AT TUKUYU OF RUNGWE

HAKIMU



azamtv

217509601

**TAARIFA KWA UMMA**

Ndugu mteja wa AzamTV, **Kuanzia tarehe 1 Agosti 2023** kutakuwa na mabadiliko ya bei kwa baadhi ya vifurushi. Kifurushi cha ***Azam Plus cha 23,000/- kitakuwa 25,000/-*** kwa mwezi, kifurushi cha *Azam Pure cha 15,000/- kitakuwa 17,000/-* kwa mwezi na Kifurushi cha ***Azam Lite cha 8,000/- kitakuwa 10,000/-.***

Kifurushi cha ***Azam Pure kwa wiki cha 5,000/- kitakuwa 6,000/-*** na kile cha **Azam Lite kwa wiki cha 2,500 kitakuwa 3,000.**

Kifurushi cha **Azam Play cha 35,000/-** kwa mwezi kitabaki vile vile bila mabadiliko.

# TUZO ZA UMAHIRI WA UANDISHI WA HABARI TANZANIA (EJAT) 2022 KATIKA PICHA



Wateule wa EJAT 2022 katika picha ya pamoja na Mgeni Rasmi, Balozi Ombeni Sefue (wa tatu kulia mstari wa mbele), Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga (kulia kwa Mgeni Rasmi), Mwakilishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Zamaradi Kawawa na Mwenyekiti wa Jopo la Majaji, Mkumbwa Ally, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Waandishi wa Habari wa Kampuni ya The Guardian Limited, Francis Kajubi (kushoto) na Sanula Athanas mara baada ya kukabidhiwa tuzo zao.



Mhariri Msanifu wa Gazeti la Nipashe, Sanula Athanas, akipokea Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Elimu toka kwa Mhadhiri wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Zakaria Malima.



Mwandishi wa Habari za Biashara wa Gazeti la The Guardian, Francis Kajubi, akipokea Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Ushirika toka kwa Kaimu Naibu Mrajisi Vyama vya Ushirika wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Consolata Kilima.

# Mabula: Mgodi Tembo Nickel utanufaisha taifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, asema mgodi wa Tembo Nickel uliopo wilayani Ngara Mkoa wa Kagera, utanufaisha taifa na wananchi wa mkoa huo.

Mabula alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Bugarama, wilayani Ngara, baada ya kutembelea eneo la mradi wa Tembo Nickel.

"Mgodi huu ni mkubwa mno na serikali ni mbia kwenye mradi huu na kwa maana hiyo ninyi pia hiyo ni mali yenu ambayo itawanufaisha kwa njia mbalimbali.

"Sisi kama serikali kuu tutakuwa tayari kutoa ushirikiano wa kutosha, Bugarama ni kata ambayo tutaneemeka kuanzia mtoto aliyezaliwa leo hadi wazee. Tunawapongeza kwa utayari wenu wa kupokea mradi huu na kwamba rasilimali zilizo Wilaya ya Ngara zinanufaisha wananchi wote," alisema Dk. Mabula.

Alisema muda wowote wananchi wanaotakiwa kupisha mradi huo watalipwa fidia ikiwa ni baada ya hatua mbalimbali za kisheria kupitiwa.

"Mmekuwa wavumilivu, lakini sasa wakati wowote mtapata fidia zenu, ile hati ya kuidhinisha watu walipwe imekamilika baada ya ninyi kuridhia kupisha mradi, lengo letu ni kuona mnawezeshwa mapema na mnakuwa na mahali pengine pa kuishi," alisema Dk. Mabula.

Aliwataka wananchi hao kushirikiana na mradi na kuulinda kwa maslahi ya serikali ambayo ni mbia katika mradi huo wa uchimbaji madini ya nikeli.

"Mradi huu ni wa ubia ambapo Serikali ya Tanzania ina hisa kwa niaba yenu, katika mradi huu kuna manufaa mengi sana mtapata, kuna watu hapa watajengewa nyumba za kisasa kabisa baada ya makazi yao kuguswa na mradi huu.

"Nyumba mtakazojengewa ni za thamani kubwa na nzuri kuliko mlizo nazo. Pia mtawezeshwa kuishi vizuri huko, mtapewa na hati ya nyumba ambazo zitawasaidia hata kukopa benki mkitaka.

Awali, akizungumza na Dk. Mabula, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Manny Ramos, alisema mgodi huo umeendelea kushirikiana na wananchi wa eneo hilo kwa kutoa ajira za kudumu na za muda mrefu huku ununuzi wake kwa asilimia kubwa ukiwa unafanywa kwenye Wilaya ya Ngara na Mkoa wa Kagera kwa ujumla.

Alisema pia wako kwenye hatua za mwisho za kulipa wananchi wanaotarajia kupisha mradi huo ili kuanza uchimbaji wa madini hayo yanayotarajiwa kunufaisha Tanzania na dunia kwa ujumla.

# Afungwa maisha kunajisi mtoto

**Na Benny Kingson,** TABORA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Uyui Katanga, imemhukumu Josephat Jackson (59), mkazi wa Kijiji cha Semembela, Tarafa ya Bukene, wilayani Nzega, kifungo cha maisha jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kunajisi mtoto mwenye umri wa miaka tisa.

Kamanda wa jeshi hilo mkoani Tabora, Richard Abwao, akitoa taarifa kwa gazeti hili alisema kuwa hukumu hiyo ni mafanikio ya Jeshi la Polisi kutokana na matukio hayo kujirudia rudia katika jamii na itakuwa fundisho.

Kamanda Abwao alisema katika Mahakama ya Wilaya ya Uyui Katanga, Adam John, alitiwa hatiani kwa kosa la kubaka na amehukumiwa kifungo cha mika 30 jela ikiwa pia ni mafanikio na wataendelea kufuatilia watu wote wenye viashiria na vitendo hivyo viovu na kuwadhibiti wasilete madhara kwa wengine.

Katika tukio lingine Kamanda alisema kuwa Julai 11, mwaka huu, katika maeneo ya Kanyeye mjini kati Manispaa na Mkoa wa Tabora, walikamata watu watatu wakiwa na pikipiki namba za usajili Mc 156 DMG na nyingine aina ya sun lg nyekundu iliyokuwa imefunikwa namba za usajii kwa gundi nyeusi na su lg rangi nyekundu MC 665 DLG, wanazozitumia kupora simu mitaani nyakati za usiku, watuhumiwa wapo mahabusu na wamefikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazo wakabili," alisema.

Kamanda Abwao, alisema kuwa Mtaa wa Musoma, Kata ya Nzega Mashariki, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora, Juni 30, 2023 walimkamata mtu mmoja akiwa na noti 10 za bandia, za 5,000 noti 9,000 na moja ya 10,000 na zimepelekwa Benki Kuu jijini Mwanza kwa utambuzi zaidi na mtuhumiwa amefikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Katika hatua nyingine Julai 19, 2023 maeneo ya Mtaa wa Mapolomoko, Kata ya Nzega Mashariki, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora, walifanikiwa kukamata watuhumiwa watatu wakiwa na televisheni nne nchi 32 na vifaa vingine vya mawasiliano.

Alisema kuwa vitu hivyo vyote ni mali ya wizi ambavyo viliibiwa Kariakoo, Kata ya Kitete, Mkoa wa Tabora, Juni 30, 2023 na watuhumiwa watatu wamekamatwa kujibu tuhuma zinazo wakabili.

Alisema kuwa jeshi lake Julai 20, 2023 maeneo ya majengo Wilaya ya Urambo, Mkoa wa Tabora, walimkamata mtuhumiwa mmoja akiwa na silaha aina ya 'shot gun' iliyotengenezwa kienyeji akiwa ameificha nyumbani kwake na alikuwa anaitumia katika uwindaji haramu na kukodisha kwa wahalifu.

Alisema kuwa Juali 10, 2023 katika Kitongoji cha Utenge Katya ya Nsenda Tarafa na Wilaya Urambo, Mkoa wa Tabora, walimkata mtuhumiwa akiwa na silaha mbili aina ya gobole ambazo zilijificha kwenye bafu lake lililojengwa kwa mabua ya mahindi na nyingine kwenye shamba lake la mahindi, mtuhumiwa anamiliki silaha kinyume na taratibu za kisheria na amefikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo.

Jeshi hilo pia limekamata kete 150 na debe tano za bangi, watuhumiwa watatu wamefikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili na wataendelea kufanya operesheni mbalimbali kuwabaini wote na kuwafikisha kwenye mkono wa sheria.

Aidha, alisema kuwa kwa kipindi cha kuanzia Mei mosi hadi Julai 13, mwaka 2023 jumla ya vijiwe 62 vya madereva wa bodaboda 1,083 walipatiwa elimu ya usalama barabarani ikiwa ni mpango mkakati wa kuzuia ajali za madereva hao ambazo zinapunguza nguvu kazi ya taifa.

Alisema jumla ya wanafunzi wa shule za msingi 88 na sekondari 52 walipewa elimu hiyo ili kuwapa mwanga na utambuzi kuhusu matumizi sahihi ya barabara na jinsi ya kuepuka ajali zisizokuwa na ulazima kwa kufuata sheria ili wawe salama wakati wote.


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**Company No. 22797**
**(the Bank)**

## NOTICE FOR CONVENING THE 26TH ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT THE 26TH ANNUAL GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 19TH AUGUST 2023 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL AND VIRTUALLY FROM 10:00 A.M. (EAT)**

The following Agenda will be transacted:

1.0 Opening Remarks, Confirmation of Quorum and Adoption of the Agenda
2.0 To Confirm Minutes of the Previous Annual General Meeting and Extra Ordinary General Meeting
3.0 To Discuss Matters Arising from the Minutes of the Previous Annual General Meeting and Extra Ordinary General Meeting
4.0 To Receive the Chairman's Statement
5.0 To Receive and Adopt the Financial Statements for the year ended 31st December, 2022 together with the Directors' and Auditors' Reports thereon
6.0 To Receive the Current Management's Report on the Operational Performance of the Bank
7.0 To Approve the Appointment of a Director
8.0 To Appoint the External Auditors for the year ending 31st December 2023 and Approve their Remuneration
9.0 To Set Date for the Next Annual General Meeting
10.0 Closing Remarks

**By Order of the Board**

Niwaeli Mziray
**Company Secretary**

**Distribution:** Shareholders - Akiba Commercial Bank Plc

**Invitees:** Board of Directors - Akiba Commercial Bank Plc
Senior Management - Akiba Commercial Bank Plc
External Auditors - KPMG
Director, Financial Sector Supervision - Bank of Tanzania

**NOTE:**

**A. PAPERS FOR THE MEETING**
Papers for the meetings will be available for collection at the Bank's Registered Offices from Monday, 14th August 2023 and at the venue on the date of the meeting.

**B. ANY OTHER BUSINESS**
Any other business to be discussed during the Annual General Meeting must be communicated to the Company Secretary not later than Monday, 14th August 2023.

**C. OPTION TO JOIN VIRTUALLY**
Shareholders may join the meeting virtually if unable to attend physically, by notifying the Company Secretary to register their virtual attendance and obtain meeting access before Thursday, 17th August 2023. The meeting can be accessed virtually only by Shareholders who have registered their attendance.

**D. ATTENDANCE BY PROXY**
A Shareholder entitled to attend and vote at these meetings may, if unable to attend in person, appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf in accordance with the provisions of the Articles of the Company.

The instrument appointing a proxy must be signed by the respective Shareholder.

The instrument appointing a proxy must be submitted to the Company Secretary at the Bank's registered office or via email by 10.00 a.m. (EAT) Thursday, 17th August 2023.

**E. TRAVEL AND ACCOMMODATION**
Each Shareholder shall be responsible for the cost of their own travel and accommodation.

**F. OTHER INFORMATION**
Shareholders are reminded to confirm/update their personal information with the Company Secretary in order to update the Company Register.

**G. CONTACT DETAILS FOR COMMUNICATION**

**Company Secretary**
**Akiba Commercial Bank Plc**
**3rd Floor, Amani Place, Ohio Street**
**P.O. Box 669**
**Dar es Salaam**

Email: cs@acbtz.com or niwaeli.mziray@acbtz.com

217504502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timu zilizopanda daraja zijiandae vizuri Ligi Kuu

**MSIMU** ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza rasmi Agosti 15, mwaka huu, kutakuwa na timu tatu zilizopanda daraja kutoka Ligi ya Championship tofauti na misimu kadhaa iliyopita ambayo mara nyingi tumekuwa tukishuhudia mbili tu.

Timu hizo ambazo zimepanda ni JKT Tanzania, Tabora United (zamani Kitayosce) na Mashujaa FC ambayo ilikuwa ya mwisho kupanda kutokana na kulazimika kucheza mechi za mchujo 'play off', kabla ya kufanikiwa kukata tiketi hiyo.

Mara nyingi tumekuwa tukiona timu mbili tu kutoka Ligi ya Championship zikipanda na hii inatokana na kutokuwa na timu yoyote iliyoweza kuifunga timu ya Ligi Kuu kwenye mechi za 'play off' mpaka Mashujaa FC ilipovunja mwiko huo kwa kuifunga Mbeya City jumla ya mabao 4-1.

Kwa maana hiyo timu tatu za Ligi Kuu zimeshuka ambazo ni Ruvu Shooting, Polisi Tanzania na Mbeya City, huku tatu toka chini zikichukua nafasi hizo na kwa bahati nzuri nyingine ni kwamba msimu uliomalizika, timu zilizoshuka daraja zote ni zile zilizokaa zaidi ya msimu mmoja kwenye Ligi Kuu.

Hiyo ni tofauti na misimu mingi ya nyuma kwani kati ya timu zinazoshuka, mbili au moja itakuwa imepanda msimu huo huo. Tuliona kwa Mbeya Kwanza msimu wa 2021/22, Mwadui, Ihefu na Gwambina msimu wa 2020/21 na mingine nyuma.

Msimu uliomalizika ulikuwa wa heri kwa timu ambazo zilipanda; Singida Fountain Gate na Ihefu, baada ya kung'ang'ana kubaki Ligi Kuu na chakufurahisha zaidi ni kwamba si kwamba zilikuja kuongeza idadi bali zilileta ushindani mkali kiasi cha Singida Fountaine Gate wakati huo ikiitwa Singida Big Stars kumaliza ikiwa nafasi ya nne na kukata tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Kwa Ihefu ambayo ilianza kwa kusuasua na kuna wakati ilikuwa inaburuza mkia, ilijitafuta mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ikafanya usajili bora ambao ulilipa na si tu kuibakisha, lakini ilimaliza ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo.

Hii inauonesha kuwa maandalizi mazuri na usajili bora ndiyo silaha ya kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na si vinginevyo, ndiyo maana tunazitaka timu zilizopanda daraja kwa sasa zisiendelee na sherehe zao za kufanikiwa kuingia Ligi Kuu, bali kufanya usajili wa maana ili kutotibua rekodi ya msimu uliomalizika kwa kutokuwa na timu yoyote iliyopanda na kuteremka kama ilivyokuwa huko nyuma.

Hatuzishauri kuwa ziache wachezaji wao waliozipandisha daraja, la hasha, lakini zikae zikijua Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa imekuwa bora jambo ambalo mataifa ya nje hata yale makubwa kisoka wanakiri hivyo. Wimbi la wachezaji kutoka mataifa mbalimbali hususan Magharibi mwa Afrika, wanaokuja kucheza soka nchini hicho ni kiashirio tosha kuwa kucheza Ligi Kuu pia kunahitaji wachezaji wazoefu ili kukabiliana na mikikimikiki.

Kwa maana hiyo, timu za JKT Tanzania, Mashujaa FC na Tabora United ziwe makini sana kwenye upembuzi yakinifu wa kusaka wachezaji bora vinginevyo na kufanya maandalizi makubwa kuepuka kurudi zilizopotoka, Championship baada ya msimu mmoja.

Zinapaswa kutambua kuwa pamoja na kufanya usajili mpya, lakini zinatakiwa kuwa na baadhi ya wachezaji ambao wamezipandisha daraja ili kutoharibu muunganiko ambao tayari zilikuwa nao kwa muda mrefu.

Kukimbilia tu kusajili wachezaji wazoefu wa Ligi Kuu ambao tayari wamepoteza ubora wao, kutazifanya zishindwe kuonyesha ushindani, lakini kudumaza vipaji vipya na damu changa ambazo tunatarajia kuziona zikija kutoa kuonesha ubora wao.

Tunataka pia kuziona zikiiga mfano wa Singida Fountaine Gate ambayo baada ya kupanda Ligi Kuu msimu mmoja uliopita, ilifanya usajili wa wachezaji bora ambao umewalipa na sasa wanaenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi wazitendee haki pesa za usajili, 'pre season'

Na Adam Fungamwango

**MARA** nyingi makocha, viongozi wa klabu na hata mashabiki wa soka nchini hulalamika sana wakati wanapoona timu zao hazitendewi haki na waamuzi katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu, Ligi ya Championship na First League.

Ukiwasikiliza wengi wao hudai kuwa klabu zinatumia gharama kubwa kwenye usajili na maandalizi ya msimu mpya (pre season), lakini cha ajabu mwamuzi anatumia dakika 90 tu kuharibu ushindi wa timu ambayo ilistahili kushinda.

Makocha wengi huwa na hoja kwenye hili, bahati mbaya tu hukutana na adhabu ya kufungiwa, lakini wanakuwa wamepeleka ujumbe kwa waamuzi na hata Bodi ya Ligi Kuu nchini (TPLB).

Kwa sasa tunaona timu zinavyopigana vikumbo huku na huko, kuzunguka dunia nzima kusaka wachezaji bora ambao zinaona watawafaa kwenye vikosi vyao. Ukiangalia hili utaona kabisa kuwa viongozi wa klabu wanatumia gharama kubwa kufanya usajili wakitegemea kufanya vema kwenye mashindano mbalimbali.

Na hata kama wakipoteza basi ionekane walistahili kupoteza kwa makocha kuzidiwa mbinu, au siku hiyo wachezaji wao hawakuwa vizuri mchezoni.

Kwa sasa klabu zimeweka kambi zingine zimesafiri kwa gharama kubwa nje ya nchi kwenda kuandaa vikosi imara vitakavyokuja kutoa upinzani mkali kwenye Ligi Kuu. Zipo zilizopiga kambi hapa hapa nchini, nje ya mikoa yao, dhamira ikiwa ni ile ile kusuka vikosi bora. Makocha nao kwa sasa wanakuna vichwa, wanatumia nguvu na akili zao zote kuwekeza mbinu na mifumo kwa wachezaji wao, wakiamini itawasaidia kupata ushindi wanapokuwa uwanjani.

Maandalizi yote na gharama zinazotumika inauma pale kiongozi au kocha anapoona timu yake imepoteza mechi kihuni kwa kulazimishwa na waamuzi kwa dhamira yao ovu, mapenzi kwa klabu husika ama vinginevyo.

Viongozi na makocha huumia sana kwani wanaona fedha na muda waliowekeza vyote ni bure, na hii mara nyingi huwakatisha sana tamaa.

Hivyo, tunapoelekea msimu mpya wa Ligi Kuu, waamuzi wawaonee huruma wachezaji, viongozi na makocha ambao wanajitoa mazoezini na kuwekeza nguvu zao na fedha, lakini wanakuja 'kupigishwa shoti' na mwamuzi kwa sababu anazozijua mwenyewe kama ni mapenzi au rushwa.

Ni wakati sasa waamuzi wakachezesha kwa haki ili mshindi apatikane yule ambaye anastahili kuupata kwa siku hiyo na si kubebana.

Cha ajabu unakuta timu imesheheni wachezaji kutoka pande mbalimbali Afrika, kikosi cha gharama kubwa, kinacheza na timu ya kawaida ambayo ina wachezaji wa kawaida sana, lakini kwa siku hiyo wakubwa wamezidiwa, ila mwamuzi hataki, badala yake atafanya kila njia kwanza kuwaondoa wachezaji wa timu ndogo kwenye mchezo kwa kuwapa kadi zisizokuwa na kichwa wala miguu na baadaye kuwamaliza kabisa ama kwa kutoa penalti isiyo halali au vyovyote vile ili mradi tu kuibeba timu kubwa.

Hali hii imekuwa ikitokea mara kwa mara kwenye ligi yetu na imekuwa ikisababisha matatizo mbalimbali, ikiwamo baadhi ya waamuzi hao hao kufungiwa, lakini viongozi, makocha na wachezaji pia kuingia kwenye mkumbo huo wa kufungiwa.

Hivi baadhi ya waamuzi wanajisikiaje wanapozionea timu ndogo ambazo zinacheza tu kwa kupambana dhidi ya timu kubwa zilizosajili wachezaji wakubwa kwa gharama?

Hatukatai, timu kubwa zishinde ila zishinde na si kubebwa. Ziachwe zifungwe ili zijipange vema kwenye mechi zinazofuata, lakini vitendo vya baadhi ya waamuzi kuanza kufanya hila ya kuzitafutia bao timu kubwa kwa njia yoyote kwenye mechi ambazo zinaonekana siku hiyo zinakaribia kukosa ushindi, si cha kiungwana na kimichezo.

Hiyo inajenga taswira kwamba timu kubwa ndizo zenye mamlaka ya kushinda na zile ndogo zipo kwenye ligi kwa ajili ya kufungwa na kugawa pointi tatu dhidi ya wenzao.

Wakati vikosi vikijiandaa na msimu mpya wa ligi, waamuzi nao wajiandae kuhakikisha watakuja kuchezesha kwa haki, wakizitendea haki gharama za usajili na 'pre season.'

## Wanawake watakiwa kuzifahamu sheria

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANAWAKE kutoka wilaya za Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro wameshauriwa kujifunza na kuzifahamu sheria mbalimbali ili waweze kuzijua haki zao za msingi zitakazowasaidia kuwa na uwezo wa kutatua migogoro inayowakabili kwa ajili ya maendeleo yao ya kiuchumi.

Mwanasheria wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Mkoa wa Morogoro, Joyce Peter, alitoa rai hiyo kwa nyakati tofauti alipotoa mafunzo yanayohusu masuala ya kisheria kuhusu Sheria ya Ardhi, Mirathi na Ndoa kwa wanawake wa Vijiji vya Minepa na Lupiro vya Wilaya ya Ulanga pamoja na Kipenyo kilichopo Wilaya ya Malinyi.

Mafunzo hayo yametolewa na Kituo cha Msaada wa Kisheria Paralegal Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na WOPATA kupitia Mradi wa POWER unaotekelezwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Malinyi na Ifakara kwa ufadhili wa Aga Khan Foundation.

Mwanasheria huyo alisema, wanawake wengi wanajikuta wanashindwa kesi kutokana na uelewa mdogo wa sheria hizo na kutofahamu wapi waende kwa ajli ya kupata huduma.

Alisema watu hawana uelewa kuhusu taratibu za umiliki wa ardhi kwa kuzingatia kulipia ada ya ardhi na kuhuisha umiliki baada ya muda wa umiliki kuisha ukiwa ni wa muda mfupi au muda mrefu.

"Tatizo kubwa nimeliona katika maeneo mengi ni migogoro ya ardhi inayotokana na uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi kwa kuingia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali na hali hiyo inasababisha malalamiko ya nani mwenye haki na eneo hilo husika," alisema Mwanasheria Joyce.

Alisema kesi zote zinazohusu masuala ya ardhi zinaanzia Baraza la Ardhi la Usuluishi kata ukiwa na vielelezo vya utambulisho wa mmiliki na baadaye kuelekea ngazi zingine ikitokea imeshindikana kufikia muafaka.

Kuhusu masuala ya ndoa na matunzo ya watoto, alisema, watu wamekuwa na kawaida ya kuishi katika dhana ya ndoa ambayo mwisho wa siku inaleta usumbufu ikitokea wamesajili ndoa zao.


Aliwataka viongozi wa vijiji kuwasaidia wanawake kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria kufikia suluhisho.

Msadizi wa Kisheria, Chediel Senzighe, alisema jamii inapaswa kufahamu na kuelewa kuandika wosia ili kuzuia watu wanaoachiwa mali baada ya mmiliki kupoteza maisha kupata usumbufu wa kupata mirathi.

"Tuandike wosia, migogoro mingi ya mirathi inatokana na marehemu kutoandika wosia na hii imepelekea familia nyingi kugombana, kupelekana mahakamani kwa kugombea mali ambazo hawajachuma wao," alisema Senzighe.

Senzighe alisema, wanawake wana haki ya kurithi na kumiliki mali kwa pamoja kati ya mke na mume na ikatokea wameachana mahakama isipate ugumu kugawa mali.

Nao baadhi ya wananchi walipata elimu hiyo akiwamo Msengeti Mpawa na Hidaya Mgalakachua kutoka Kijiji cha Kipenyo Wilaya ya Malinyi kwa nyakati tofauti walisema elimu waliyopewa imewapa uelewa mpana katika kufahamu sheria mbalimbali watakuwa walimu wazuri kwa wananchi wenzao.



Mwanzilishi wa Taasisi ya CAReH Africa, Profesa Gbenga Ogedebde wa Chuo Kikuu cha NYU Grossman (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa makoti ya kuvaa madaktari wanapokuwa kazini kwa Mtafiti Mwandamizi wa Kituo cha Afya cha Ifakara, Dk. Jerry Hella (katikati), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Prof. Chinwe Ogedebde kutoka Chuo Kikuu cha Tiba Hackensack, Marekani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyuo vikuu 15 bora Malasyia kuonyesha fursa masomo Dar

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu vikubwa 15 vya nchini Malaysia vinatarajia kufanya maonyesho hapa nchini kwa lengo la kuwaonyesha Watanzania fursa mbalimbali za kielimu zinazopatikana kwenye vyuo hivyo.

Maonyesho hayo yatafanyika kwenye hoteli ya Verde Zanzibar Julai 28 - 31, mwaka huu kwenye hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam kuanzia asubuhi mpaka jioni.

Kwa mujibu wa mratibu wa maonyesho hayo kwa hapa nchini, Abdulmalik Mollel, maonyesho hayo yataratibiwa na Education Malaysia Global Services (EMGS) ambayo ni wakala wa Serikali ya Malaysia.

Mollel alisema vyuo vikuu hivyo ndivyo vikuu bora nchini Malaysia na wanafunzi wanaotarajia kupata matokeo ya kidato cha sita, wale waliopata matokeo yao na wale waliokwishapata matokeo yao ya astashahada ndiyo wakati wao wa kupiga simu na kutafuta fursa hiyo.

Mollel alisema hiyo ni fursa kwa watu wanaotaka kusoma cheti, Stashahada, Shahada za Uzamili na Shahada ya Uzamivu (PhD) nao wanapaswa kuchangamikia fursa hiyo adimu ya kukutana na vyuo hivyo.

Alisema vyuo vikuu vya hapa nchini ambavyo vinahitaji ushirikiano na vyuo vikuu nchini Malaysia vinapaswa kutumia fursa hiyo kutafuta maeneo ya uhusiano kwenye taaluma mbalimbali.

"Vyuo vikuu vinapaswa kuchangamkia fursa kulingana na uhusiano wanaouhitaji, je, ni uhusiano kuhusu kozi za uhandisi, kozi za biashara, afya, exchange programu za wanafunzi, je, ni kuhusu kuendeleza wahadhiri? Hii ndiyo fursa yenyewe ya kuitumia," alisema Mollel.

Aidha, alisema ujio wa maonyesho hayo pia ni fursa kwa taasisi mbalimbali ambazo zingependa wafanyakazi wake kwenda kuongeza kiwango chao cha elimu nchini Malaysia kwenye fani mbalimbali katika kiwango cha Shahada ya kwanza, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamivu (PhD).

"Kuna watu wako kazini na wangependa kuongeza ujuzi na pengine wangependa kuongeza ujuzi wao nchini Malaysia sasa vyuo vikuu hivyo vitakuwa hapa kwa hiyo taasisi hizo ama ni za serikali au binafsi hii ndiyo fursa ya kuitumia," alisema Mollel.

"Inawezekana kukawa kuna taasisi binafsi na umma zenye fursa mbalimbali kama chuo cha aviation, ambao wanataka kukutana na wenye vyuo hivyo moja kwa wao waseme muda huu ili siku vitakapokuja waweze kutumia muda wao vizuri," alisema.

Alisema taasisi za fedha ambazo zimekuwa zikikopesha wanafunzi wa elimu ya juu Zanzibar na Tanzania Bara, NGOs mbalimbali zinazosaidia wanafunzi wanatakiwa kujua kwamba huu ndiyo muda wao wa kuwasiliana na vyuo hivyo ili iwerahisi kukutana nao watakapowasili hapa nchini.

Mollel alisema kuna mawakala mbalimbali wa elimu ya juu nje ya nchi walioko hapa nchini na wale nchi za Zambia, Rwanda, Malawi, Burundi na Kenya wanapaswa kuja nchini kuzungumza na wawakilishi wa vyuo hivyo kwa tarehe watakazokuwa nchini.

"Kwa mfano maonyesho haya hayataanzia hapa Tanzania, yataanzia Kenya kwa hiyo mawakala wa Kenya wanaweza wakaenda moja kwa moja wakafanya booking ya kukutana nao na mawakala wa Tanzania wanaotaka kupeleka wanafunzi Malaysia tena kwenye vyuo ambavyo mwanafunzi anaweza kuanzisha Malaysia akamalizia Canada, au akaanzisha Malaysia akamalizia Marekani au Uingereza," alisema.

"Au vyuo vikuu hapa nchini ambavyo vinataka kuanzisha programu za ushirikiano kwamba mwanafunzi anaweza kusomea Tanzania miaka fulani na akasomea Malaysia miaka flani hizi ni miongoni mwa fursa ambazo vyuo vya Tanzania hazipaswi kuzikosa," alisema.

Alisema wakuu wa shule za sekondari wanapaswa kufanya mawasiliano ya namna wanavyoweza kukutana na wawakilishi wa vyuo hivyo kwani kutokana na wingi wa wanafunzi kuna uwezekano wengine wakakosa fursa ya kuonana na vyuo hivyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga (katikati), akitabasamu baada ya kukata utepe kufungua tawi jipya la Benki ya CRDB katika kisiwa cha Mafia mwishoni mwa wiki. Kulia ni Ofisa Mkuu Biashara, Boma Raballa na kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Zephania Sumaye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka wananchi wachangamkie fursa za benki kuepuka mikopo umiza

**Na Mwandishi Wetu,**
MAFIA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amewataka wananchi kutumia huduma za benki ili kuepuka mikopo yenye riba kubwa inayowafanya baadhi washindwe kuilipa, hivyo kupoteza mali zao.

Kipanga alitoa rai hiyo alipozindua tawi la Benki ya CRDB mwishoni mwa wiki wilayani Mafia mkoani Pwani.

Alikumbusha kuwa serikali inatekeleza mpango wa kuwajumuisha wananchi wengi zaidi katika huduma rasmi za fedha kwa kushirikiana na taasisi za fedha ili kuwapa unafuu utakaochangia maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

"Fedha ni kichocheo muhimu cha maendeleo hivyo ukuaji wa sekta ya hii nchini ni muhimu sana katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

"Ili sekta ya fedha itoe mchango unaokusudiwa, inapaswa kuwa imara na yenye uwezo wa kuwafikia wateja wengi mjini na vijijini kama inavyofanya Benki ya CRDB kufungua matawi kila kona ya nchi.

"Ninawasihi wananchi wenzangu tutumie huduma za benki kuepuka mikopo ya mtaani yenye riba kubwa sana," alihimiza Kipanga.

Naibu Waziri huyo pia alizikumbusha taasisi za fedha kuweka masharti na vigezo nafuu ikiwamo kutoza riba nafuu ili kuwashawishi watu wengi zaidi kunufaika na mikopo inayotolewa ili waachane na ile inayotolewa mtaani ambako riba yake hufika mpaka asilimia 50 na mwisho wa siku kujikuta katika matatizo yasiyo ya lazima.

"Benki ndicho chombo kikuu cha kutolea huduma za kifedha kwa wananchi. Benki zinatakiwa zizingatie mahitaji ya wananchi na zitoe hamasa kwa wananchi kutambua umuhimu wa kutumia huduma za benki kwa maendeleo binafsi na ya taifa letu kwa ujumla wake.

"Kwa kutumia huduma za benki siyo tu mwananchi anaweza kupata mkopo nafuu bali fedha zake zinakuwa salama na urahisi wa kufanya miamala kwa saa 24," alisema Kipanga ambaye ni Mbunge wa Mafia.

Kipanga alisisitiza hayo baada ya Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, kusema benki yao ndiyo inaongoza kwa mtandao mkubwa zaidi nchini na wanazo huduma rafiki kwa wananchi ikiwamo programu ya Imbeju inayotoa mikopo wezeshi kwa vijana na wanawake wenye biashara changa ambazo hazijakidhi vigezo vya kukopesheka kwa masharti ya kibiashara.

"Wanawake na vijana wa Mafia nanyi fursa hii imewafikia. Benki ya CRDB ipo hapa ili kukidhi mahitaji yenu ya kifedha. Licha ya mikopo mnayoweza kuomba pamoja na kujiwekea akiba, benki yetu inatoa ushauri wa kuhusu biashara na uwekezaji. Njooni tuwape huduma kwa viwango vya kimataifa," alisema Raballa.

Mbali na Imbeju, Raballa alisema Benki ya CRDB inatoa mikopo ya biashara na ujasiriamali katika sekta tofauti, akizitolea mfano kilimo, uvuvi na ujenzi wa nyumba.

Alisema kwa sasa benki hiyo imeiboresha programu yake ya benki kwa simu (simbanking). Sasa inatoa rukhsan kwa mteja kufanya mambo mengi zaidi ikiwamo kulipia bili za mara kwa mara, kulipa marejesho kama anao mkopo au kutuma fedha kwa wapenda wake kwa tarehe ya mbele atakayoipanga.

"Simbanking yetu ya sasa inatumia akili bandia kuratibu huduma na ukiwa na programu hii unaweza kutuma maoni yako na yakafanyiwa kazi kwa wakati. Tumewekeza sana katika mifumo ya kidijiti ili kurahisisha huduma kwa wateja wetu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Zephania Sumaye, alisema kuimarika kwa huduma za fedha wilayani mwake kunafungua fursa nyingi za biashara na uwekezaji.

"Mafia ni kisiwa cha utalii. Hapa kuna historia kubwa kuhusu maendeleo na ustaraabu wa binadamu. Tunawakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kuja kuzitumia fursa kemkem zilizopo," alisema Sumaye.

## Serikali yaahidi kuunga mkono kampeni kukabili VVU/Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, amesema serikali itaendelea kuunga mkono kampeni ya GGML KiliChallenge inayolenga kuchangisha fedha kwa ajili ya kuendeleza mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Amesema kampeni hiyo inakwenda sambamba na jitihada za serikali kutokomeza maambukizi mapya ya ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Pia amemwagiza Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo kuhakikisha wanafunzi wawili wenye umri wa miaka 14 waliopanda Mlima Kilimanjaro kwa siku saba kupitia kampeni hiyo iliyoasisiwa miaka 22 iliyopita, kuingizwa katika orodha ya watu watakaohudhuria Sikukuu ya Mashujaa ambayo itafanyika kesho mkoani Dodoma.

Kampeni hiyo iliyoasisiwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) mwaka 2002, pia inalenga kuisaidia serikali kutimiza malengo ya kitaifa ya kufikia sifuri tatu - kutokuwa na maambukizi mapya, kutokuwa na unyanyapaa na ubaguzi, na kutokuwa na vifo vitokanavyo na Ukimwi.

Akizungumza katika hafla ya kuwapokea washiriki 35 waliopanda Mlima Kilimanjaro na 26 waliouzunguka mlima huo kwa baiskeli mwishoni mwa wiki wilayani Moshi, Jenista alisema GGML imeonyesha ushujaa kuratibu kampeni hiyo kwa miaka 22.

"Kwa hiyo, GGML imejitoa kubeba maumivu ya siku saba kwa ajili ya maumivu ya Watanzania, hili jambo la kijasiri, la kishujaa litaendelea kukaa katika vitabu vya mambo ya msingi yaliyofanywa na taasisi zetu nchini. Kwa mfano huu mzuri ulioonyeshwa na GGML, ninapenda kuwaambia hongereni sana," alipongeza.

Alitoa wito kwa mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa kuiga mfano wa GGML katika kutoa huduma kwa jamii kwa moyo wa dhati na kujitoa.

Aliwapongeza washiriki pamoja na watoto hao waliopanda mlima tarehe 14 Julai mwaka huu na kushuka tarehe 20 Julai na kusisitiza kuwa ni mashujaa ambao mafanikio yao yamedhihirisha kuwa mwitikio dhidi ya VVU na Ukimwi unawezekana iwapo kutakuwa na dhamira ya dhati kwa kila Mtanzania kutokomeza janga hilo nchini.

Mwanafunzi aliyefanikiwa kupanda Mlima Kilimanjaro na kufika katika Kilele cha Uhuru, Rebecca Damiani (14), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kivukoni.

Abel Musa (14), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mbugani alishindwa kufika Kilele cha Uhuru baada ya kuugua malaria akiwa mlimani.

Waziri Jenista alisema watoto hao wameonyesha uzalendo mkubwa kwa Taifa kwa kujitosa kuungana na Watanzania wengine katika kuchochea nguvu ya mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU, hivyo wanapaswa kutambuliwa kama mashujaa katika nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, aliishukuru serikali kwa kuunga mkono katika mapambano hayo na kuhakikisha zinapatikana fedha kwa ajili ya kutokomeza janga la Ukimwi nchini.

Pia aliwapongeza watoto hao kwa rekodi ya kipekee waliyoiweka na kuahidi kuwa GGML itaendelea kuwaunga mkono katika kutimiza ndoto zao.

Kaimu Mkurugenzi TACAIDS, Jerome Kamwela, aliwapongeza wapanda mlima hao na kusema wamekuwa mabalozi wazuri katika kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU nchini.



## Serikali kujenga kituo kikubwa cha waraibu dawa za kulevya

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI ina mpango wa kujenga kituo kikubwa cha huduma za utengamao kwa waraibu jijini Dodoma ili waweze kupata mafunzo ya ujasiriamali katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Hayo yalisemwa juzi na Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kitengo cha Tiba na Huduma za Utengamao, Dk. Cassian Nyandindi, kwenye warsha ya waraibu waliopata nafuu kwa mkoani Tanga ili waweze kuwaibua wenzao kujiunga na huduma za tiba na utengemao.

Alisema mamlaka hiyo ni taasisi ya serikali iliyo chini ya Waziri Mkuu inayoshughulia na kuratibu masuala yanayohusiana na tatizo la dawa za kulevya hapa nchini.

Alisema hatua hiyo ni moja ya jitihada za dhati zinazofanywa na serikali kupanua na kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini, huku akieleza kwa sasa wana jumla ya vituo 15 vinavyohudumia zaidi ya watu 14,500.

"Lakini mikakati yetu ni kupanua huduma hizo ili kuweza kuwafikia waraibu wengi zaidi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, lengo likiwa ni waweze kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Alisema kwamba serikali inawasaidia waraibu waweze kupata mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo mbalimbali ili waweze kujikimu na kukuza pato la taifa hiyo ndio mikakati ya serikali katika kupanua huduma hizo za utengamao nchini.

Akizungumzia kuhusu vituo cha waraibu hapa nchini alisema vinasaidia waraibu kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya kupata matibabu mbalimbali yakiwamo ya UKIMWI, kifua kikuu, homa ya ini pamoja na matatizo ya akili.

Alisema pia wanaoenda kwenye vituo hivyo wanapata fursa ya kupata wasanii wanaowabadilisha tabia na wanaweza kuachana na tabia za waraibu kupunguza uhalifu, kuimarisha mahusiano kwenye ngazi ya jamii na kupata mafunzo ya ujasiriamali.

Katibu Mtendaji wa Asasi ya Gift Of Hope, Saidi Bandawe, alisema kwamba walikuwa na kikao kazi na wadau mbalimbali na jamii wanayokwenda kuiwezesha kwa ajili ya kufanya huduma kwa ajili ya watumiaji wa dawa za kulevya.

Alisema wao kama asasi wameamua kukutana kwenye kikao hicho na wadau mbalimbali ili kuifanya wanaporudi kwenye maeneo yao wawe na watetezi kwa ushirikiano na wanaotumia dawa za kulevya kuwapeleka kwenye huduma.

Wilaya ambazo zimeshiriki kwenye warsha hiyo ni Tanga, Pangani, Mkinga, Muheza pamoja na Korogwe kutokana na uwepo wa wahitaji wengi kupata huduma hiyo.

Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga, Abdurhaman Shillow, akizungumza wakati akifungua warsha hiyo alisema kwamba Tanga hawafurahii kuona wanakuwa nafasi ya pili kwa matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini.

# Vijiji 4 vyaruhusiwa kutekeleza mradi majaribio wildlife credit

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

BARAZA la Halmashauri Kuu ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet WMA, imebariki vijiji vinne vinavyozunguka ushoroba wa kitendeni ulioko mpakani mwa Tanzania na Kenya kutekeleza mradi wa majaribio wa Wildlife Credit maarufu kama tuzo.

Pia limewaelekeza wanachama wake kuhakikisha viashiria vyote hatarishi kwa ushoroba huo vinadhibitiwa na kuimarika.

Meneja wa Enduimet WMA, Igno Laitayok, akizungumza jana na wakazi wa vijiji vya Lerang'wa na Kitendeni katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, alisema baada ya ujio wa mradi huo hawategemei kuona wanachama wao wanaendelea kufanya uharibifu wa ushoroba huo, hasa ukataji miti ya mitarakwa na misandale, ambayo husafirishwa kinyemela kwenda nchi jirani.

Laitayok, alikuwa akizungumza na wananchi hao wakati wa utambulisho wa mradi huo wa majaribio wa Wildlife Credit, unaotekelezwa na Shirika la World Wildlife Fund (WWF).

"Hatutegemei kwamba tutapata hizi fedha, halafu ujangili kwenye eneo la ushoroba unaendelea. Wakati tunaendelea kumaliza mitarakwa (miti), kukata miti kwa ajili ya kujengea maboma ya mifugo. Lakini miti ya misandale inaharibiwa sana kwa kukatwa; tunaendelea kuona inakatwa na kuendelea kupelekwa nchi jirani.

"Tunategemea kwamba vile viashiria vyote ambavyo ni hatarishi kwa hii shoroba, tuhakikishe kwamba tunadhibiti. Tunataka kuona matokeo ya kweli yanayoonekana na kupimika kutokana na kuhifadhi hii shoroba. Kwa kufanikiwa vile viashiria kuonekana, sasa hizi pesa ambazo WWF wamesema watatoa, ndipo zitakapokuja kwenye kijiji."

Kwa mujibu wa Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT Transboundary Landscape (Southern Kenya, Northern Tanzania), Prof. Noah Sitati, vijiji vinne vya Irkaswa, Kitendeni, Lerang'wa na Kamwanga, ndivyo vilivyochaguliwa kuingia katika mradi huo wa majaribio wa miezi 18, kabla ya kutumika katika shoroba nyingine zote nchini.

Mradi huo wa Wildlife Credit, unalenga zaidi kutoa motisha ya utunzaji na ulinzi wa ushoroba wa kitendeni, ambao ni mapito ya wanyamapori wanaohama, kati ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) na Amboseli ya nchini Kenya, kutafuta malisho na maji.

"Leo sisi tumekuja kuwasilisha mradi hapa kwenu Lerangwa na Kitendeni na hatujui ninyi mnataka kufanya nini baada ya kupata hizi pesa za tuzo. Kazi yetu ni kuwajulisha tu juu ya mradi, lakini haya mambo yote ambayo mnazungumza ninyi, mtaketi chini na kukubaliana kwa vile tunajua mnaweza mkabadili kipaumbele chenu ni kipi.

"Mkiketi ninyi wenyewe mtaamua kwamba hii pesa tuliyopata WWF tufanyie nini. mkitaka zahanati, nyumba za madaktari mtaamua wenyewe," alisema.

Meneja Mradi wa Wildlife Credit, Frank Damson, alisema: "Tumeweka vigezo katika sehemu nne za Mradi wa Wildlife Credit, tutaangalia kwenye wildlife (wanyamapori), tutangalia habitat (mazingira), tutaangalia governance (utawala bora) na kuna njia tofauti za kupima hizo indicators (viashiria).

...Tutaangalia kuna dashboard (kanzidata) ambayo itatengenezwa kuweza kupima kwa kupiga picha za satellite, kuangalia ushoroba ukoje. Tunafanya huu mradi kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Enduimet WMA."



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Daniel Chongolo, akizungumza na wakazi wa Jiji la Arusha waliojitokeza jana katika mkutano mkuu wa chama hicho kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Kanda ya Kaskazini, ulitoa fursa kwa baadhi ya viongozi wa chama hicho kuzungumza na wananchi wa jiji hilo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Watumishi Hospitali ya Bombo wapewa mafunzo ya utapiamlo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAFUNZO maalumu yanayohusu matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto yametolewa kwa watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo ya siku mbili jana, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo, Dk. Mohamed Salehe alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza ufanisi wakati wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

Dk. Mohamed ambaye ni Mkuu wa Idara ya Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga alisema baada ya kumalizika kwa mafunzo hayo anaimani kwamba washiriki wanakwenda kuwa chachu katika utoaji wa huduma.

Mafunzo hayo yamewashirikisha wataalamu mbalimbali wakiwamo kutoka Ustawi wa Jamii, madaktari, manesi na maofisa lishe ambayo yanatajwa kwamba yatakuwa chachu katika utoaji wa huduma. Alisema mafunzo hayo yanatolewa kwa nadharia na vitendo huku washiriki wakionekana kuwa na uelewa mzuri na walimu wamekuwa wakitoa mafunzo ya kuwaezesha kutoa matibabu kwa watoto wenye utapiamlo.

Alisema: "Unapomtibu mtoto mwenye tatizo la utapiamlo linahitaji watu wote waweze kusaidiana na chimbuko la hasa na sababu kuweza kujulikana na kumtibu ndio moja njia pekee ya kuweza kumwondolea huyo mtoto tatizo hilo."


"Pamoja na kwamba wanatibiwa hospitali wanahitaji matunzo huko nyumbani watoto wanakaa na wazazi hivyo ni kuwapa mafunzo ya namna ya kuwalea watoto kama hao kwani wanaweza kuwa kama wengine na ndoto zao ila mafunzo kwa wazazi ni jambo la muhimu," alisema.

Ofisa Lishe wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga –Bombo, Imakula Mwamrefu, alisema wapo kwenye mafunzo maalumu yanayohusu matibabu kwa watoto wenye utapiamlo mkali wanaozaliwa katika hospitali hiyo.

Alisema kwamba kwenye hospitali hiyo wana kitengo ndani ya wodi ya watoto 13 na 14 kinachohusika kwa matibabu ya utapiamlo mkali kwa Watoto, hivyo kutokana na hilo wameona wawe na mafunzo ya kujengeana uwezo namna ya kuwatibu watoto wanapofika hospitalini.

Hata hivyo alisema mafunzo hayo yatakuwa kwa njia ya kuelekezana na vitendo kuona namna ya kutambua utapiamlo mkali.

Naye Daktari wa Wodi ya Watoto katika hospitali hiyo, Dk. Mwalimu Khalid, alisema mafunzo hayo ya matibabu kwa watoto wenye utapiamlo mkali ni muhimu kutokana na kwamba wanakuwa na miili yenye mabadiliko, hivyo kuna utofauti jinsi ya kuwatibu ukilinganisha na wale wa kawaida.



# TANROADS yatumia bil.12.6/- ujenzi, ukarabati wa barabara

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Miba Ndilimbi, amesema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 wamepokea Sh.bilioni 12.6 katika Mfuko wa Barabara na kutumika katika ujenzi.

Aidha, amesema fedha hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kero ya ubovu wa barabara ikiwa matumizi yake yalisaidia pia katika ujenzi wa madaraja na makaravati ambayo yalikuwa yakisababisha kujaa kwa maji barabarani na kufanya magari yashindwe kupita.

Mhandisi Ndilimbi alibainisha hayo hivi karibuni wakati akizungumza na Nipashe kuhusu juhudi za serikali katika kuondoa kero za barabara korofi mkoani humo.

Alieleza kuwa katika Mkoa wa Shinyanga wanahudumia mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,177.4 ambako kati ya hizo barabara za changarawe ni km 917.22 na za lami ni km 260.52 kwa mkoa wote.

Alisema kupitia fedha hizo za mfuko wa barabara walifanya matengenezo katika Barabara ya Mwabomba, Bugomba 'A' Bulugwa, Butibu ambako katika Halmashauri ya Ushetu walifanya matengenezo ya barabara yenye urefu wa km 70.49 kwenye maeneo korofi.

Kadhalika alieleza kuwa katika barabara hizo waliweka, makaravati pamoja na kuchonga mitaro ambapo walitumia Sh. milioni 329 ambazo zilitolewa kupitia fedha za maendeleo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Flying Construction Co Ltd inayotekeleza ujenzi wa barabara hiyo, Idd Iyombe, alisema kuwa kabla ya ujenzi wa Karavati la Mwabomba kipindi cha masika maji yalikuwa yanapita juu ya daraja na kusababisha barabara hiyo kutopitika.

Aidha, baadhi ya wakazi wa Kata ya Mwabomba akiwamo Scolastika Wishi waliishukuru serikali kwa kujenga karavati akisema litawasaidia kusafiri na kupita kwa usalama wakati wote.

Alisema pia itawasaidia kuondokana na adha ya wananchi kusombwa na maji wakati wa masika, sambamba na kusafirisha mazao yao na malighafi kwenda kwenye masoko.



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), akiwa kwenye ziara yake ya kukagua ujenzi wa miradi ya maji Bugarama, Wilaya ya Msalala Mkoa wa Shinyanga unaotarajiwa kukamilika hivi karibuni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Vijana wakumbushwa kuunda vikundi ili kupata mikopo

**Na Timothy Itembe,** MARA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Juliana Masaburi, amewataka vijana kutumia fursa ya kuunda vikundi vya kijamii ili waweze kuinua vipato vyao ikiwa ni pamoja na kupatiwa mikopo ya riba nafuu.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akijibu maswali ya papo kwa papo yaliyoulizwa na baadhi ya vijana kutoka Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) katika ziara yake ya kikazi wilayani Tarime na kusema kuwa ili kujikwamua kiuchumi vikundi havikwepeki.

"Lengo la vikundi hivi ni kujipatia mikopo pamoja na fursa mbalimbali za kimaendeleo zitakazowasaidia kutoka katika wimbi la umaskini na kuondokana na kuwa tegemezi," alisema.

Aidha, baada ya mkutano huo, Masaburi alichangia mashine ya kufyatua matofali kwa vijana hao lakini akaomba kupatiwa makubaliano ya mkataba wa utekelezaji wa mradi.

Neye Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya Tarime, Godfrey Gotora, aliwataka vijana kubuni miradi ya kuwapatia fedha za kuendeshea maisha badala ya kukaa bila kazi.

Pia, aliwaonya kutotumiwa na baadhi ya viongozi wasiokuwa na maadili kuwachafua viongozi wengine ambapo alisema kuwa hiyo ni moja ya mmomonyoko wa maadili.

Kadhalika, aliwataka vijana hao kuwa na nidhamu kwa viongozi wa ngazi ya serikali na chama na kuwatahadharisha kuepuka kutumika kuwachafua kwenye mitandao ya kijamii viongozi waliopo madarakani.

**Neye Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya Tarime, Godfrey Gotora, aliwataka vijana kubuni miradi ya kuwapatia fedha za kuendeshea maisha badala ya kukaa bila kazi.**

# 'Serikali iongeza ushirikishwaji katika mipango ya maendeleo'

**Restuta Damian,** KAGERA

WAJUMBE wa kikao cha Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 mkoani Kagera wameiomba serikali kuongeza ushirikishwaji katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Pia wameomba kuboreshwa kwa fursa za rasilimali zinazotazamiwa kulinyanyua taifa kiuchumi kwa miaka 25 ijayo.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha uelimishaji umma ngazi ya mkoa juu ya Dira ya Taifa ya mwaka 2050 ikiwa na lengo la kukuza uchumi wa nchi na pato la mwananchi mmoja mmoja.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wajumbe hao, Seleman Idrisa, alisema ili kuinua pato la uchumi wa taifa na mwananchi mmoja mmoja ni lazima kuwapo na mipango shirikishi yenye kuangalia makundi yote ambayo yatakuwa msaada wa kufika Dira ya Taifa ya mwaka 2050.

Alisema katika jamii kila Mtanzania anawajibu wa kushughulika na kufikisha taifa katika uchumi endelevu kupitia shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na uwekezaji katika sekta mbalimbali.

"Mfano katika Mkoa wa Kagera zipo fursa za kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi hizi zikiangaliwa kwa kufanya uboreshaji hata katika mikoa mingine ambayo hufanya uzalishaji tufafikia dira inayokusudiwa," alisema Idrisa.

Naye mfanyabiashara kutoka mkoani Kagera, Nicolaus Bashekaki alisema, jumuiya za wafanyabiashara wanatakiwa washirikishwe katika mipango ya taifa ya kibiashara kwani matokeo ya mipango hiyo inatekelezwa juu yao.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa alisema, Mkoa wa Kagera, unahitaji rasilimali fedha itakazosaidia kuinua vipato vya halmashauri hususani katika makusanyo.

Alisema kwa miaka 10 Mkoa wa Kagera umekuwa wa mwisho kwenye maendeleo hali inayolazimu kila halmshauri kupangiwa bajeti kulingana na ukusanyaji wake.

Alisema ukusanyaji wa mapato kwa mwaka ni Sh.bilioni 1.5 ambayo hutumika kufanya matumizi mbalimbali kwenye ofisi za umma.

"Hiki ni kiwango cha chini kabisa ambacho kinafanywa na mfanyabiashara mdogo akifanya kwa jitihada kubwa lakini hapa unaambiwa ni kipato cha mkoa," alisema Mwassa.

Aidha, alisema, Dira ya Taifa inapopanga mipango inatakiwa iweke kipaumbele kwenye mikoa ambayo imeachwa nyuma kimaendeleo ili nayo iweze kuinuka kiuchumi.

Mhandisi Mkuu kutoka Wizara ya Fedha, Omari Athuman, alisema, serikali ina mipango ya uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 inayotegemea maoni ya wananchi ili kutimiza takwa la ushirikishwaji.

Hata hivyo alisema, ili kuongeza mafanikio yaliyopatikana kwa dira iliyoishia mwaka 2025 na kuongeza nyingine ya mwaka 2050 ni lazima kutumia rasilimali zilizopo nchini na ushirikishwaji wa wananchi katika kuyafikia malengo hayo.

# Nipashe Spotika



**KLABU TANO ZILIZOFANYA USAJILI BORA HADI SASA 12 - 13**



Fred

# WACHEZAJI 6 WANAOSTAHILI KUUZWA MANCHESTER UTD

**MANCHESTER, England**

WAKATI dirisha la usajili la majira ya joto likizidi kupamba moto, Manchester United inajikuta katika njia panda kwenye harakati zake za kuwafikia wenye nguvu. Ili kuimarisha kikosi, 'Mashetani Wekundu' hawana budi kuzingatia si tu kupata vipaji vipya bali pia kuwaondoa baadhi ya wachezaji.

Mengi yamesemwa kuhusu wanaotarajiwa kusajiliwa na Manchester United katika msimu huu wa majira ya joto. Katika makala haya, tunawaangalia wachezaji sita ambao 'Mashetani Wekundu' hao wanatakiwa kuwauza ili kurahisisha orodha yao mpya...

**#6. Anthony Martial**

Baada ya kuwa na wakati mgumu alipotolewa kwa mkopo kule Sevilla, Anthony Martial, ameendelea kukatisha tamaa kwa Manchester United. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa anaendelea kuwa pasua kichwa kwa kocha Erik ten Hag na anaongoza orodha hii ya wanaohitajika kuuzwa.

Kiwango cha Mfaransa huyo wakati alipokuwa Old Trafford kimekuwa si cha kuridhishwa na sasa unaweza kuwa wakati wa kuanza upya. Kumuuza Martial si tu kutaiingizia fedha nyingi, bali pia malipo yake makubwa ya mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki ni sawa na matumizi yasiyo na tija.

**#5. Fred**

Fred amekuwa na wakati mgumu kupata uthabiti wowote katika Klabu ya Manchester United tangu aliposajiliwa hapo mwaka 2018. Usajili wa hivi karibuni wa Mason Mount unamaanisha kuwa atakuwa na muda mchache wa kucheza na kuongeza ushindani kwenye safu ya kiungo, na hivyo kudumaza maendeleo ya Mbrazil huyo.

Huku akiwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa katika klabu hiyo, itakuwa ni kwa manufaa kwa mchezaji na klabu kuachana. Ofa ya Galatasaray ilikataliwa na Manchester United kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil kama ilivyoripotiwa na Fabrizio Romano na amekuwa pia akiwaniwa na klabu za Saudi Arabia na Fulham.

**#4. Jadon Sancho**

Jadon Sancho amekuwa duni tangu arejee England, na hivyo kuzuia kiwango cha juu kilichotarajiwa kutoka kwa mchezaji huyo cha pauni milioni 75. Ingawa fowadi huyo ameonesha machache juu ya uwezo wake siku za nyuma, muda wake Manchester United kwa ujumla umekuwa wa kukatisha tamaa. Idadi yake ya mabao 12 katika mechi 79 alizocheza kwenye ligi hiyo ni mbaya kutokana na mchezaji anayelipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Sancho amekuwa akihusishwa na kurejea Borussia Dortmund, huku Tottenham Hotspur na Brighton & Hove Albion zikimwania katika kipindi hiki cha majira ya joto. Raia huyo wa England ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi pale Old Trafford huku akiwa hana kiwango cha kuvutia. Manchester United itafanya vema kama itaamua kumuuza.

**#3. Brandon Williams**

Brandon Williams alipoingia uwanjani alionekana kama tegemeo la kusisimua, akionesha uwezo wake mwingi kama beki wa pembeni na winga. Hata hivyo, ujio wa Erik ten Hag umemfanya kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza cha Manchester United.

Williams ameona muda wake wa kucheza ukipungua kwa kiasi kikubwa na hakuna dalili za kuona kama muda utaongezeka. Uhamisho wa kudumu kwa klabu ambapo anaweza kupata dakika za kawaida itakuwa na manufaa kwa maendeleo yake. Beki huyo wa England anazidi kuonekana kutoshiriki katika mipango ya Man United.

**#2. Harry Maguire**

Maisha ya Harry Maguire katika Klabu ya Manchester United yametatizwa tangu alipowasili kutoka Leicester City kwa mkataba wa rekodi ya dunia wa pauni milioni 80, mwaka 2019. Ingawa nyota huyo wa kimataifa wa England ana kipaji kisichopingika, amekuwa na ugumu kuingia kwenye kikosi cha kwanza chini ya kocha Erik ten Hag.

Kwa uwapo wa Lisandro Martinez na Raphael Varane wanaopendelewa zaidi na kocha, itakuwa bora kwa Maguire kuhama. 'Mashetani Wekundu' hao wameripotiwa kutaka kumpiga bei kiasi cha pauni milioni 50, huku klabu ya Tottenham Hotspur ikijatwa kumuwania.


**#1. Donny van de Beek**

Donny van de Beek aliwasili Manchester United akiwa na matarajio makubwa kutoka Ajax ambako alikuwa chini ya kocha wa sasa Erik ten Hag. Hata hivyo, kiungo huyo wa kati wa Uholanzi amekuwa na wakati mgumu kufanya mabadiliko na amejitahidi kupata utimamu wa mwili au kujiamini.

Inaweza kuwa manufaa kwa pande zote mbili kuachana na kumruhusu Van de Beek kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

## ISIKUPITE

KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, hawa ndio mabeki 10 bora wa kati kwa sasa; Ruben Dias (Man City), Josko Gvardiol (RB Leipzig), David Alaba (Madrid), William Saliba (Arsenal), Eder Militao (Madrid), Virgil van Dijk (Liverpool), Lisandro Martinez (Man United), Alessandro Bastoni (Inter) na Kim Min-jae (Bayern).



Extra Time

# KLABU TANO ZILIZOFANYA USAJILI BORA HADI SASA



Jurrien Timber

**LONDON, England**

DIRISHA la uhamisho wa majira ya joto linaweza kuwa kipindi kigumu kwa klabu. Ingawa ni lazima kufanya usajili ambao unaweza kuimarisha vikosi vyao, lakini zinapaswa kuhakikisha uwiano ndani ya timu hauvurugiki.

Klabu pia zinahitaji kuuza wachezaji ili kukaa ndani ya vigezo vya haki sawa za kifedha (Financial Fairplay) na pia kutoa fedha kwa wachezaji wapya.

Baadhi ya klabu zitahitajika kuhakikisha kuondoka kwa nyota hakuleti doa katika mipango yao ya siku za usoni. Ili kufanya hivyo, zitahitaji kuajiri kwa kuwajibika na kwa busara.

Kwa hiyo, dirisha la usajili linakuja na seti yake ya matatizo ambayo yanahitaji akili kali na hatua thabiti.

Ndio maana mambo mengi yanapaswa kuzingatiwa kabla ya kupanga biashara ya upande wowote kwenye dirisha la usajili la majira ya joto. Sasa hebu tuangalie klabu tano zilizofanya biashara bora katika soko la uhamisho hadi sasa.

**#5. Liverpool**

Baada ya msimu mbaya wa 2022-23, Liverpool walitarajiwa kuwa makini na wenye busara katika dirisha la usajili la majira haya ya joto. Wanaonekana kuishi kulingana na matarajio hayo. Kupata saini ya Alexis Mac Allister kutoka Brighton & Hove Albion kwa euro milioni 42 tu ili kuwa kazi nzuri kabisa.

Waliimarisha zaidi safu yao ya kiungo kwa kumsajili kiungo mchanga na anayetumainiwa, Dominik Szoboszlai kutoka RB Leipzig kwa euro milioni 70. Nahodha huyo wa Hungary ni mwanasoka hodari ambaye anaweza kucheza katika nafasi kadhaa na anaweza kuwa nyenzo ya thamani kwa kikosi cha kocha Jurgen Klopp.

Liverpool pia wameweza kuondoa baadhi ya wachezaji katika klabu hiyo. Wachezaji kama James Milner, Naby Keita na Roberto Firmino wameondoka bila malipo huku Fabio Carvalho, Calvin Ramsay na Rhys Williams wakitolewa kwa mkopo.

Alex Oxlade-Chamberlain ni mchezaji mwingine ambaye mkataba wake ulimalizika Juni lakini bado hajapata klabu mpya.

**#4. Real Madrid**

Real Madrid wamejiwekea kikomo kwa kufanya uhamisho wa kimahesabu sana kwa hivi karibuni. Ndivyo ilivyo kwa shughuli zao msimu huu wa majira ya joto. 'Los Blancos' hao wametumia rasilimali zao kwa kuwajibika. Kumsajili Jude Bellingham kwa mkataba wa thamani ya euro milioni 103 bila shaka kunaonekana kama hatari inayostahili kuchukuliwa.

Pia wamefanikiwa kupata huduma ya kiungo chipukizi, Arda Guler kutoka Fenerbahce kwa euro milioni 20 na pia wamemnasa beki wa kushoto, Fran Garcia kutoka Rayo Vallecano kwa euro milioni tano.

Kumsajili Joselu kutoka Espanyol kwa mkopo kulivutia sana kwani licha ya Espanyol kushuka daraja msimu uliopita, Joselu aliwafanyia kazi nzuri. Alifunga mara 16 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu uliopita na anaonekana kuwa mbadala mzuri na wa bei nafuu wa Karim Benzema.

Mbali na Benzema, wachezaji kama Marco Asensio, Eden Hazard na Mariano Diaz wameondoka katika klabu hiyo.

**#3. Paris Saint-Germain**

Kama kila msimu wa majira ya joto, Paris Saint-Germain wamefanya tena usajili wa hali ya juu wakati huu. Wamemsajili Lucas Hernandez kutoka Bayern Munich kwa euro milioni 45. Beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 27, ataimarisha safu yao ya ulinzi pamoja na Milan Skriniar, ambaye amesajiliwa kwa uhamisho huru.

PSG pia wamemnunua Manuel Ugarte kutoka Sporting Lisbon kwa euro milioni 60 na Marcos Asensio kwa uhamisho huru. Kang-in Lee mwenye umri wa miaka 22, kwa euro milioni 22 anawakilisha ununuzi wa busara pia na PSG wamepata saini ya Hugo Ekitike kwa euro milioni 28.5.

Kwa upande wa kuondoka, Lionel Messi na Sergio Ramos wameondoka katika klabu hiyo baada ya misimu miwili na hiyo itakuwa ahueni kubwa katika masuala ya kifedha kwa PSG. Junior Dina Ebimbe ameuzwa kwa Eintracht Frankfurt kwa euro milioni 6.5.

**#2. Arsenal**

Washambuliaji wa Arsenal walikuwa katika kiwango kizuri msimu uliopita. Kai Havertz atakuwa nyongeza nzuri sana kwa mstari huo wa mbele na nguvu zake na harakati bora. Zaidi ya hayo, ni makaratasi machache tu ambayo yanasimama katika njia ya usajili bora zaidi kwa 'Washikabunduki' hao.

Kwanza, wamekubali mkataba na West Ham United kwa Declan Rice wenye thamani ya euro milioni 120 mahali fulani kwenye uwanja wa mpira. Rice ni mmoja wa viungo chipukizi bora zaidi barani Ulaya na atakuwa nyongeza nzuri kwenye safu ya kiungo ya Arsenal.

Pili, kuwasili kwa Jurrien Timber kutoka Ajax kunaripotiwa kuwa karibu na atakuwa chaguo bora katika safu ya beki wa kati. Arsenal walionekana nyuma katika kipindi cha pili baada ya William Saliba kupata jeraha na kuwasili kwa beki huyo wa kati wa Ajax kutaongeza ubora katika safu yao ya ulinzi.

Granit Xhaka, mtu anayependwa, ameondoka kwenye klabu hiyo. Alijiunga na Bayer Leverkusen kwa dili la euro milioni 25. Pablo Mari aliuzwa kwa Monza kwa euro milioni 4.9 na Ainsley Maitland-Niles bado ni mchezaji huru baada ya kuona mkataba wake ikimalizika mwishoni mwa Juni.

**#1. Inter Miami**

Imekuwa rahisi sana linapokuja suala la Inter Miami na dirisha la uhamisho wa majira ya joto. Kwa sasa wako mkiani mwa jedwali katika ukanda wa kutoka East Conference kwenye Ligi Kuu ya Marekani (MLS), na wanahitaji muujiza kushughulikia mambo na kufuzu kwa mchujo.

Ni mapema sana kuwafuta kwa sababu wamesaini wachezaji wawili ambao pia ni wachezaji waliocheza pamoja hapo awali.

Tunawataja Lionel Messi na Sergio Busquets. Wachezaji wote wawili wamesajiliwa kwa uhamisho huru. Ingawa inaweza kusemwa kwamba, Messi na Busquets wamepita kwenye ubora wao, wawili hao bado wana mengi ya kutoa katika kiwango cha juu zaidi kwenye mchezo huo.

Baada ya yote, Messi aliiwezesha Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka jana tu na pia alikuwa mmoja wa wachezaji bora wa PSG katika ushindi wao wa Ligue 1.


Busquets alianza michezo 28 ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku Barcelona wakishinda taji hilo msimu uliopita. Inatosha kusema, usajili wa hawa wawili unaweza kuibadilisha Inter Miami.

## Nukuu

"Harry alinipongeza kwa uchaguzi wa nahodha mpya na akasema ana furaha sana kwangu. Ninaelewa nafasi yake si bora kwa sasa. Inapaswa kuwa ngumu kwake lakini alikuwa na wakati mzuri na mimi. Lazima iwe ngumu kwake,**" Bruno Fernandes, alifichua alichoambiwa na Harry Maguire baada ya kupoteza unahodha wa Manchester United.**



"Tuna (makombe) mengi mwaka huu. Tuna matumaini ya kushinda mataji yote, tunajua itakuwa ngumu, lakini tuna timu nzuri, kocha na wachezaji wapya. Matamanio ni sawa na mwaka jana na tunatazamia kuwa na msimu mzuri. Bila shaka, tunataka kushinda mataji kadhaa mwaka huu, ngoja tuone kitakachotokea,**" Nyota wa Al-Nassr, Cristiano Ronaldo.**



"Nilizungumza na Kyle na kila kitu kiko sawa - kwa hivyo sasa tutaona kitakachotokea. Lakini siwezi kukuambia chochote kwa sababu bado anafikiria kuhusu hilo. Joao yuko hapa na amekuwa muhimu kwetu siku za nyuma. Amerejea na sehemu ya kundi, kwa hivyo tutaona kitakachotokea. Nadhani mambo mengi yatatokea. Siwezi kujibu ni kwa sababu sijui,**" Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, alipoulizwa kuhusu Kyle Walker, Bernardo Silva na Aymeric Laporte, endapo wataondoka Etihad majira haya ya joto.**





Wachezaji wa Simba, Clatous Chama na Fabrice Ngoma, wakiwa mazoezini nchini Uturuki kujiandaa na msimu mpya wa mashindano 2023/24.

# KLABU ZILIZOTOKA KUSAKA 'UBANI' MSIMU 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

KIPINDI hiki cha maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, kila klabu ya Ligi Kuu imekuwa na mipango yake.

"Pre season' hii tumeshuhudia timu nyingi zikiamua kuondoka sehemu ambayo zimezoea kwenda kuweka kambi mbali na yalipo makao makuu yao, ingawa zipo zilizoamua kuendelea kukaa hapo hapo kutokana na mipango yao.

Viongozi kadhaa walipohojiwa sababu za kwenda kuweka kambi mbali, walisema ni kuwafanya wachezaji wawe watulivu, kubadilisha mandhari na kutosumbuliwa na ndugu na jamaa kwa shida ambazo wakati mwingine hazihitaji hata mtu kutoka kambini kwenda nyumbani. Wengine wakasema wanatafuta maeneo yenye vifaa bora, hali ya hewa, viwanja na hata kupata mechi bora za kirafiki.

Katika makala haya tumekusanya taarifa za vikosi mbalimbali ambavyo vimeamua kwenda mbali na kwao kwa ajili ya maandalizi ya msimu unajao...

**Simba - Uturuki**

Ilikuwa ni Julai 10 wakati wachezaji wa Simba, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi walipoondoka nchini kwenda Ankara, Uturuki kwa ajili ya kambi ya siku 21.

Ingawa walioondoka awali walikuwa ni 17 tu, lakini mpaka kufikia jana karibuni wachezaji wote walikuwa wameshawasili kambini isipokuwa Luis Miquissone.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amebainisha kuwa leo hii kikosi hicho huenda kikawa na mechi ya kwanza ya kirafiki.

Simba ndiyo timu pekee nchini kwenye 'pre season' ya msimu huu ambayo imekwenda kupiga kambi barani Ulaya, ikijiandaa na michuano ya African Football League, Ligi ya Mabingwa Afrika, Ligi Kuu Tanzania Bara, Ngao ya Jamii, Kombe la FA na lile la Mapinduzi.

**Azam FC - Tunisia**

Azam FC ilikuwa ndiyo timu ya kwanza kuanza 'pre season' msimu huu, ikiondoka nchini kwenda Tunisia kwenye Jiji la Sousse kwa ajili ya maandalizi yake msimu ujao.

Iliondoka nchini Julai 8 ikiwa na watu wasiopungua 40, wakiwamo wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na wafanyakazi na tayari imeshacheza mechi tatu za kirafiki.

Mechi ya kwanza ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na ikachapwa idadi ya mabao kama hayo na Esperance ya huko, kabla ya juzi usiku ikiichapa US Monastir mabao 2-1.

Ofisa Habari, Hasheem Ibwe amesema aina ya mechi wanazocheza ndiyo sababu iliyowafanya wao kusafiri kutoka Tanzania kwenda Tunisia.

"Tunacheza na timu kubwa barani Afrika ambazo zinafanya vema kwenye michuano ya kimataifa, hivyo tulihitaji kujipima nazo nguvu kwani nasi tunakwenda kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika," alisema Ibwe.

Wakati Simba ikiwa timu pekee nchini kwenda kuweka kambi Ulaya, Azam nayo ni timu pekee iliyoweka nje ya Tanzania, Tunisia.

**Singida Fountaine Gate - Arusha**

Wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye michuamo ya Kombe la Shirikisho, Singida Fountaine Gate, wao wakaamua kutoka kwao Singida kwenda kuweka kambi jijini Arusha.

"Tunaweka kambi hapa kwa siku 14, programu ya mwalimu Hans Van Pluijm ni ya wiki mbili kwa mujibu wake tukiwa hapa, baada ya hapo tutarudi Singida kwa ajili ya tamasha la Singida Day, halafu tunaanza safari ya Tanga kwenda kwenye Ngao ya Jamii," alisema Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza.

"Kwanza hata msimu uliopita tulifanyia mazoezi hapa hapa, kwa hiyo tuna uzoefu napo, tutafanya maandalizi yaliyokuwa mazuri pamoja na hali ya hewa yake kuwa ya baridi sana naamini mambo yatakwenda sawa tu," alisema winga wa timu hiyo, Deus Kaseke.

**Namungo FC - Arusha**

Kikosi cha Namungo chenye maskani yake mkoani Lindi nacho kikaamua kuondoka kwenye Makao Makuu yao kuelekea jijini Arusha kuweka kambi kwenye kituo cha Black Rhino Academy.

Namungo ina kazi kubwa ya kurejesha makali yake ya misimu kadhaa iliyopita, kwani haikuwa na matokeo ya kuridhisha msimu uliomalizika.

Mashujaa FC - Zanzibar

Hii ni timu ambayo itaanza kucheza Ligi Kuu msimu huu baada ya kupanda kwa mara ya kwanza, ikiwa na maskani yake mjini Kigoma.

Hata hivyo, imesafiri kutoka huko kwenda visiwani, mjini Zanzibar kuweka kambi kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Kuu.

"Tunapenda kuwataarifu kwamba, maandalizi ya msimu ujao kwa klabu yetu yatafanyikia visiwani Zanzibar," ilisema taarifa ya klabu hiyo, huku ikitajwa kuwa kocha mpya, Mohamed Abdallaah 'Bares' ndiye aliyependekeza kikosi hicho kwenda kuweka kambi huko.

**Dodoma Jiji - Iringa**

Klabu ya Dodoma Jiji, yenyewe imetoka makao makuu ya nchi na kwenda kujichimbia mkoani Iringa kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Kassim Liogope, anasema wameweka kambi mkoani Iringa ambapo pamoja na mambo mengine, hali ya hewa ya huko ni ya baridi hivyo inaruhusu wachezaji kufanya mazoezi kwa muda mrefu.

"Hali ya hewa nzuri, uwanja mzuri, yaani yale mahitaji yote ya 'pre season' tuliyokuwa tunayahitaji yamepatikana hapa na ndiyo maana tumechagua kuja Iringa, kulikuwa na sehemu kama tatu tulizipendekeza, lakini mwisho wa siku hapa ndipo tumepachagua kwa sababu kumekidhi vigezo ambavyo sisi kama benchi la ufundi tulikuwa tumependekeza vipatikane," anasema kocha huyo.

**JE, WAJUA?**




TIMU nane zitakazoshiriki michuano ya Soka Afrika (African Football League), Al Ahly, Mamelodi Sundowns, Wydad Casablanca, ES Tunis, Simba, TP Mazembe, Petro Luanda na Enyimba, zitacheza mechi moja tu (nyumbani na ugenini) na endapo zitapata matokeo ya jumla zitafuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Zingine zote zitalazimika kucheza raundi mbili nyumbani na ugenini (mechi nne) ili kufuzu hatua ya makundi.





# 'Uwekezaji wa sekta ya afya kuitangaza Tanzania kimataifa'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), Dk. Alphonce Chandika, amesema uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika sekta ya afya nchini kumefanikisha azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Tanzania kuwa na utalii wa kimatibabu.

Dk. Chandika alibainisha hayo juzi jijini hapa alipotembelewa na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma waliokwenda kumpongeza kwa huduma bora za matibabu ya kibingwa ambazo zinatolewa hivi sasa katika hospitali hiyo ambazo zimesaidia kupunguza gharama za kusafiri kwenda India.

Alisema yeye kama kiongozi wa hospitali hiyo anaishukuru serikali kwa kuwekeza katika sekta ya afya hususani katika hospitali hiyo hali ambayo imewezesha kupokea wagonjwa kwa ajili ya matibabu ya kibingwa kutoka ndani na nje ya nchi.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kupata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya matibabu ya kibingwa na kupunguza gharama ambazo Watanzania walikuwa wanalazimika kuzitumia kusafiri kwenda India na mataifa mengine kwa ajili ya kufuata matibabu, lakini pia inawezesha azma ya Rais Samia ya nchi yetu kuwa na utalii wa kimatibabu.

"Hivi sasa tunapokea watu mbalimbali kutoka mataifa kama vile Comoro, Kenya, DRC Congo na mataifa mengine mengi ambayo wanakuja kupata huduma zetu za kimatibabu katika hospitali yetu ya Benjamini Mkapa," alisema Dk. Chandika. Aidha, aliishukuru Jumuiya Maridhiano Mkoa wa Dodoma ambayo inaundwa na viongozi wa dini mbalimbali mkoani hapa kwa kitendo chao cha kuwapongeza kwa namna ambavyo wanatoa huduma kwa wananchi.

"Hichi mlichokifanya kimetutia moyo sana na kinatufanya kuongeza juhudi zetu katika kuwahudumia wananchi ili kuokoa maisha yao, mlikuwa hamna ulazima wa kuja kutupongeza lakini hiki mlichotufanyia leo ni jambo kubwa sana kwetu tunawashukuru sana," alisisitiza Dk. Chandika.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God, alisema lengo la kufika katika hospitali hiyo ni kumpongeza Rais Samia pamoja na watumishi wa hospitali hiyo kwa huduma bora wanazozitoa kwa wananchi.

"Mimi niliwahi kulazwa hapa na nilikuwa katika hali mbaya lakini kutokana na huduma zilizopo hapa vifaa tiba pamoja na madaktari na wauguzi wanaojituma ilipata huduma bora na kunisaidia kupona lakini kama isingekuwa hospitali hii nilipaswa kupelekwa India kwa matibabu hivyo namshukuru sana Rais wetu pamoja na watumishi wa hospitali hii," alisema Askofu Dk. Chande.

Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Alice Kaijage, aliwapongeza watumishi wa hospitali hiyo kwa namna ambavyo wanaiwakilisha vizuri serikali katika kutekeleza Ilani ya uchaguzi kwa kutoa huduma bora za kimatibabu.

Alisema: "Niwapongeze sana kwa hiki ambacho viongozi hawa wa dini wamekisema kuwa hospitali hii inatoa huduma bora za kimatibabu lakini pia hii yote ni kwa sababu ya utashi wa Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan kuwekeza kwenye sekta ya afya," alisema Dk. Kaijage.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili Rais Samia amefanya mambo mengi ya kuwezesha watumishi wa umma ikiwamo kuboresha maslahi yao kwa kulipa malimbikizo ya mishahara pamoja na kupandishwa kwa madaraja.

Alisema: "Kwa muda mrefu sana wakongwe kwenye utumishi wa umma mtakuwa mnakumbuka watumishi tulikuwa na shida sana kwenye madai ya malimbikizo ya mishahara yetu lakini kwa muda mfupi Rais Samia amelipa malimbikizo ya mishahara Sh. bilioni 199, madeni ya likizo Sh. bilioni 42 na kupandisha madaraja watumishi 135,170".



Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano wa Mkoa wa Dodoma waliomtembelea juzi kwa ajili ya kuishukuru serikali na watumishi wake kutokana na huduma za afya wanazozitoa kwa wagonjwa wote bila kujali itikadi yoyote. Kulia ni Mwakilishi wa Wafanyakazi Bungeni, Dk. Alice Kaijage, (wa pili kushoto) Katibu wa BAKWATA Dodoma, Shehe Husseni Kuzungu na (wa tatu kulia) Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Watumishi H/shauri Singida watakiwa kujenga ushirikiano

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATUMISHI wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida wametakiwa kujenga ushirikiano kwa kuanzisha mtandao wa mawasiliano kikazi ili kwenda na kasi inayofanana katika utekelezaji wa majukumu na hasa usimamizi wa miradi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema wakati wa kikao kazi ambacho kiliwashirikisha wakuu wa shule za sekondari, walimu wakuu, waratibu elimu kata, watendaji wa kata na wakuu wa idara na vitengo.

Alisema ili kufikia malengo ya taasisi kuna kila sababu ya kuwapo mtandao kazi baina ya watumishi, hasa wanaotekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo ili kubadilishana uzoefu lakini kupeana mbinu za kufikia malengo ya mradi kwa wakati likiwamo suala la ubunifu.

Jeshi aliwapongeza walimu wakuu kwa usimamizi mzuri wa miradi ya boost pamoja na ile iliyopata fedha kutoka serikali kuu na kusema mafanikio hayo ni matokeo ya ushirikiano kati yao na watumishi walioko chini yao lakini na jamii katika kata husika.

Aliwataka walimu wakuu wa shule za msingi pamoja na wakuu wa shule za sekondari zilizopata fedha kuzingatia suala la uwazi kwa kuhakikisha taarifa za utekelezaji wa mradi pamoja na taarifa ya fedha zinakuwepo wakati wowote zitakapohitajika.

Pia, aliwataka watumishi hao kusimamia suala la nidhamu kwao kama viongozi na kwa watumishi waliopo chini yao, kutatua kero za wananchi pamoja na kero za watumishi wanaowaongoza kwa wakati lakini pia kusimamia suala zima la ukusanyaji.

# Viongozi kata, vijiji wahimizwa kutoa taarifa sahihi za CAG

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MRATIBU wa Mtandao wa Asasi ya Kiraia Wilaya ya Dodoma (NGONEDO), Edward Mbogo, amewataka watendaji wa kata, vijiji, vitongoji kutoa taarifa sahihi za utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa wananchi ili wapate uelewa.

Alisema taarifa hizo ni zile zinazohusu sekta za miradi mbalimbali ikiwamo ya elimu ambayo inayogusa miundombinu inayotumia njia ya PETS, kupitia mradi wenye jina la Audit Accountability Initiative Project (AAI) katika Wilaya ya Bahi.

Mbogo alisema hayo juzi kwenye mkutano wa kuwasilishwa taarifa rasmi ya Kamati ya Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (PETS) kwa Shule ya Mindola na Chilungulu uliofanyika Wilaya ya Bahi.

Aliwataka viongozi hao kutoka ngazi ya kata, vijiji na vitongoji kuwa wawazi kwa wananchi wao kuhusu taarifa zinazotolewa na CAG inayohusiana na miradi ambayo inayofanyika ikiwamo inayotekelezwa ya elimu.

Alisema miradi hiyo inayotekelezwa lazima iwe wazi kwa kuwa inalenga kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wananchi na hata kwa upande wa watendaji na viongozi katika kuboresha miundombinu ya shule za msingi na madarasa yaliyopo.

"Lengo kuu la mradi huo ni kuboresha mawasiliano ya mapendekezo ya CAG na kuongeza ushiriki wa wadau na viongozi wa ngazi ya halmashauri za wilaya na vijiji katika kuchochea serikali kuongeza juhudi kutekeleza mapendekezo ya CAG katika halmashauri," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Donald Mejitii, alisema kuwa wataendelea kutoa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa mradi wa uwajibikaji kijamii.

Mejitii alisema ujio wa mradi huo ni fursa kubwa kwa Wilaya ya Bahi ambao unaotekelezwa na Mtandao wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Dodoma (Ngonedo).

Ofisa Miradi wa Ngonedo, Luhaga Makunja, alisema walengwa wa mradi huo walikuwa ni wananchi wa Wilaya ya Bahi ambao maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii yanategemea zaidi ubora wa huduma zinazotolewa na halmashauri za wilaya.



# CCM yashtukia ufisadi kwenye ujenzi uzio mnada wa mifugo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imeshtukia ufisadi kwenye ujenzi wa uzio wa mnada wa mifugo katika Kijiji cha Sipa kilichopo Kata ya Kambikatoto wilayani Chunya.

Aidha, wizara hiyo inadaiwa kuujenga mnada huo bila kuwashirikisha viongozi wa Mkoa wa Mbeya wala wa Wilaya ya Chunya jambo ambalo limezua maswali miongoni mwa wajumbe wa kamati hiyo.

Uzio huo unadaiwa kujengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa zaidi ya Sh. milioni 300, huku ukiwa hauna miundombinu muhimu ikiwamo vyoo, ofisi, sehemu ya kupumzikia pamoja na josho.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Chunya, Benedicto Matogo, alisema mnada huo ulijengwa kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo wa eneo hilo.

Alisema awali walikuwa wanauzia kwenye eneo la wazi ambalo lilikuwa ni hatarishi na ndipo wakaiomba wizara iwasaidie na kwamba tangu mwanzo mpaka mwisho mradi ulisimamiwa moja kwa moja na wizara.

Eneo lililozungushiwa uzio huo lina ukubwa wa ekari 20 na kwamba mnada wa mifugo unafanyika kila Jumatatu ambapo wanapokea wastani wa ng'ombe 200 mpaka 250 na mbuzi kati ya 60 na 100.

"Sisi hatukuwahi kushiriki kwenye ujenzi huu, wizara ilimtafuta mkandarasi yenyewe na fedha zote ilikuwa inalipa yenyewe, sisi kama halmashauri tulipokabidhiwa tulibaini kuwa na mapungufu ambayo tulimtaka mkandarasi kurekebisha," alisema Matogo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka alisema wizara ilikabidhi mradi huo kwa wananchi ukiwa na mapungufu mbalimbali hali ambayo iliwapa wasiwasi.

Alisema kwenye mnada huo hauna miundombinu muhimu lakini wataalamu wa Wizara walishakabidhi kwa wananchi na tayari umeshaanza kutumika.

Alisema ofisi yake haina taarifa yoyote muhimu kuhusu ujenzi wa mradi huo licha ya kwamba umejengwa ndani ya wilaya yake na hivyo akaiomba kamati kuwasaidia.

"Fedha hizi ni za wananchi na sisi sote tunajenga taifa moja lakini hizi tabia za kuviziana siyo nzuri, mradi umejengwa ndani ya wilaya lakini hatuna taarifa yoyote, wala hatuwezi kuelezea kwamba mpangokazi wake unaonyesha patakuwa na nini," alisema Mayeka.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alisema wananchi wa eneo hilo wanafurahia uzio huo kujengwa bila kujali uhalisia wake kutokana na mazingira waliyokuwapo awali.

Alisema hata yeye hajawahi kushirikishwa kuhusu ujenzi wa mnada huo zaidi ya kusikia kutoka kwa wananchi na viongozi wa kijiji hapo na kwamba alipofika alijua bado ujenzi unaendelea lakini akaambiwa na wananchi kwamba wameshakabidhiwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, alisema kamati hiyo haiwezi kuupokea mradi huo kutokana na kutoendana na thamani ya fedha zinazotajwa kutumika.

Aliitaka Wizara ya Mifugo kufuatilia na kuwashughulikia watu wote waliofanya hujuma kwenye mradi huo na kwamba wasipofanya hivyo chama kitawashtaki kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Lakini pamoja na kwamba mradi huu ulikuwa unatekelezwa na wizara, viongozi wa Wilaya ya Chunya na wa Mkoa hamjatekeleza wajibu wenu ipasavyo, hamkutoa malalamiko yenu mkasema potelea mbali, siyo sahihi kabisa," alisema Dk. Mwakajumilo.

Alisema kwa namna walivyofanya tathmini ya mradi huo ni kwamba una thamani ya Sh. milioni 20 na siyo Sh. milioni 300 kama ambavyo wataalamu walisema.

Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi inaendelea na ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali za mkoa huo ambapo leo inaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya baada ya kumaliza Chunya.



Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo (kulia), akipokea taarifa ya ujenzi wa Shule ya Msingi Mafyeko, kwa Revocatus Mgongo wakati akiwa katika ziara ya Kamati ya Siasa ya Mkoa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TARURA yapewa siku 7 kukarabati barabara ya Igazo-Igodima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, umepewa wiki moja kukarabati Barabara ya Igazo-Igodima ili wananchi waendelee kuitumia wakati taratibu zingine zinafuata.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi kwenye Kata ya Igazo ambapo baadhi ya wananchi walisema barabara hiyo ni mbovu na wanashindwa kusafirisha mazao yao.

Aliwataka wananchi wa eneo hilo kutoa taarifa ofsini kwake endapo wataalamu hao hawatafika katika eneo hilo kwa ajili ya kurekebisha barabara hiyo.

"Wakati mnasubiri hizo taratibu zenu zingine pitisheni kwanza greda hapa likwangue ili wananchi wasihangaike, hawa wananchi wa Igodima wanategemea huduma huku chini na hawa wa Iganzo wanalima huko milimani sasa wanahitaji kusafirisha mazao yao," alisema Malisa.

Baadhi ya wananchi walisema wanashindwa kusafirisha mazao yao kwa kutumia magari kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu na hivyo wanalazimika kusafirisha kwa kutumia punda.

Mmoja wa wananchi hao, Abida Franco alisema wamiliki wa magari wanagoma kupandisha na magari yao kwenda kubeba mazao kwa kuhofia kuharibu magari yao.

Alisema hata pikipiki na bajaji hazipiti kirahisi kwenye barabara hiyo kutokana na kuwa na makorongo ambayo yanahatarisha vyombo vyao.

# Ugonjwa mtoto wa jicho wahatarisha maisha wakazi Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unakabiliwa na ongezeko la ugonjwa wa mtoto wa jicho ambapo zaidi ya asilimia 50 ya watu wanaougua macho na kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wamebainika kuwa na tatizo hilo.

Mratibu wa huduma za macho wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Fariji Killewa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa madaktari bingwa wa macho kutoka nchini Ujerumani.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wananchi waliojitokeza katika hospitali hiyo wakiugua macho walikuwa 2,399 lakini waliobainika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho walikuwa 1,499.

Alisema watu hao walipatiwa matibabu ya tatizo hilo kwa kufanyiwa upasuaji na kwamba tatizo hilo ni kubwa katika maeneo mengi lakini uelewa wa wananchi ni mdogo.

"Tatizo hilo linaendana sana na umri, huwa unawakumba watu wenye umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea, lakini wengi huwa wanachelewa kujitokeza kupata matibabu kwa hiyo nawashauri wananchi wawe wanajitokeza.

Alisema madaktari bingwa wa macho kutoka Ujerumani, wanatarajiwa kuweka kambi ya wiki moja katika hospitali hiyo kuanzia Agosti 22 mpaka 29 mwaka huu na kwamba watashirikiana na wataalamu waliopo kuwatibu watu watakaojitokeza.

Alisema kampeni hiyo ya kupima macho inaratibiwa kwa ushirikiano kati ya hospitali hiyo na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, kupitia taasisi yake ya Maryprisca Wemen Foundation.

Ofisa Habari wa hospitali hiyo, Agrey Mwaijande, alisema huduma hizo zitatolewa bure kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kupata huduma hiyo.

Alisema waliamua kuanzisha kampeni hiyo ya kuhamasisha wananchi baada ya kubaini kuwa baadhi ya watu wamekuwa wakishindwa kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa sababu ya kuogopa gharama.

Alisema wengi wamekuwa wakijifungia majumbani bila kutibiwa hali ambayo inaweza ikawasababishia upofu ambao ni tatizo kubwa zaidi.

"Tumebaini kwamba baadhi ya watu wanaogopa kuja kupata huduma hii kwa sababu ya gharama, sasa tuwaombe sana wajitokeze wakati wa kambi yetu ili watibiwe, watakaobainika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho watafanyiwa upasuaji," alisema Mwaijande.

Kwa upande wake mwakilishi Taasisi ya Maryprisca Women Foundation, Fatuma Bora, alisema kampeni hiyo inawahusu wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya na hivyo akawataka wajitokeze.

Alisema matatizo ya macho mtu asipotibiwa mapema anaweza akapata upofu wa kudumu na hivyo likawa ni tatizo zaidi, hivyo akawataka kuwahi kupata matibabu.





## 'Huduma ya mobile kliniki italeta huduma bora'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema ubora wa vifaa vya huduma ya mobile kliniki utasaidia kupata huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa basi jipya la huduma za ZOP Mobile clinic, lenye thamani ya Sh. milioni 140 katika Uwanja wa Maisara Mjini Zanzibar.

Alisema nyezo hizo zitasaidia kutoa matibabu ya afya katika viwango vya hali ya juu na kuoka maisha ya wananchi kutokana na nia waliyoonyesha siku zilizopita.

Aidha, alisema uchunguzi wa afya mapema ndiyo njia pekee ya kuepukana na maradhi mengi mwilini, hivyo jamii inapaswa kutumia kliniki za ZOP na vituo vingine vya afya kulinda afya zao.

Waziri huyo, alieleza kuwa Wizara ya Afya itaendelea kutoa ushirikiano na msada unaostahiki kwa taasisi zinazojitoa kuwapatia matibabu ya afya wananchi ili kuokoa maisha yao.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa maradhi yasioambukiza alisema, takribani watu milioni 18 wamefariki duniani kwa maradhi ya saratani, ambapo Zanzibar inakadiriwa kuwa na wagongwa 2,000.

Aidha, aliitaka jamii kuhakikisha watoto wakike wenye umri kati ya miaka 14 hadi 17 kupatiwa chanjo ya kinga ili kupunguza tatizo la saratani Zanzibar.

Awali Katibu Mkuu wa Zanzibar, Outreach Program (ZOP), Dk. Naufal Kassim Haidar, alisema wamepata mabadiliko makubwa katika taasisi na jamii kutokana na kumiliki mabasi matatu ya kutolea huduma za afya Zanzibar.

Aidha, alipongeza Serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano mzuri wanaotoa kwa taasisi binafsi sambamba na kusamehe asilimia 50 ya ushuru wa bandari wakati wa kusafirisha gari hilo.

Akisoma risala katika sherehe hiyo, Mwenyekiti Kamati ya Utendaji Zanzibar Outreach Program, ZOP, Wahid Kassim Mohammed, aliahidi kutunza basi hilo ili kudumu muda mrefu sambamba na kuitaka jamii kujitokeza kwa wingi wakati wa kambi ili kupata huduma.

Kiongozi wa Shirika la Lions kutoka Ujerumani, Kanda ya Tanzania, Happiness Nkuya, alisema, wameamua kutoa msaada wa basi hilo kwa ZOP kutokana na huduma wanazotoa kwa jamii.

# Dk. Mwinyi kutoa ofisi, bajaji kwa watoa msaada wa sheria

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kutoa majengo ya ofisi pamoja na usafiri wa bajaji kwa watoa huduma za msaada wa kisheria Zanzibar ili kuwawezesha kuwafikia wananchi wengi wanaohitaji huduma hiyo.

Rais Mwinyi alitoa ahadi hiyo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya nne ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema serikali yake inakwenda kuchukua hatua hiyo haraka kutokana na ukweli kuwa huduma za msaada wa kisheria ni kiungo muhimu cha upatikanaji wa haki nchini hasa kwa wananchi wasio na uwezo wa fedha pindi wanapohitaji msaada wa kisheria.

"Nimeelezwa kuwa wasaidizi wa kisheria wanahitaji majengo ya ofisi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao vizuri. Lakini wanaomba usafiri wa bajaji, hawa watu hawana makubwa pengine wangetaka kuomba magari. Hivyo mie nalichukua na serikali inakwenda kulishughulikia haraka.

"Najua tuna mambo mengi lakini ni muhimu sana kwa ajili ya kujenga mazingira bora ya wao kutekeleza majukumu yao." Alisema.

Saleh Mussa Alawi, ambaye aliwasilisha hotuba kwa niaba ya wasaidizi wa kisheria alisema kuwa wasaidizi wa kisheria walio wengi visiwani humo hawana mejengo binafsi ya ofisi pamoja na usafiri kuweza kuwafikia watu mbalimbali katika jamii ambao wanahitaji huduma za msaada wa kisheria.

Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Legal Services Facility (LSF), Jaji Mstaafu Robert Makaramba, alisema ushirikiano kati ya serikali na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria ikiwamo wasaidizi wa kisheria ni nyenzo muhimu ya kujenga mazingira mazuri ya wasaidizi wa kisheria na sekta kwa ujumla.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi), Raphael Nombo, akizungumza na wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (hawapo pichani), wakati akifunga kikao cha faragha cha bodi hiyo kilichofanyika mkoani Singida. Kushoto kwake ni Kaimu Meneja Mfuko wa Barabara, Mhandisi Rashid Kalimbaga na Meneja Msaidizi, Utawala na Fedha wa Bodi, John Aswile. **PICHA: NEEMA EMANNUEL**

## Wakulima, wajasiriamali wahimizwa kulima mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mwani nchini, wakulima na wajasiriamali wa mwani pamoja na wadau wametakiwa kuelekeza nguvu katika kulima zao hilo kutokana na kukua kwa thamani pamoja na fursa zinazotokana na zao hilo.

Wito huo umetolewa na Muhando, Waziri kutoka Taasisi ya Zanzibar Milele Foundation wakati wa programu ya ziara ya kutembelea mashamba ya wakulima wa mwani visiwani humo iliyofanyika Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza zaidi na kuona ni namna gani zao la mwani linavyolimwa na kusarifishwa Zanzibar katika kuleta tija na kuongeza kipato kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Aidha, alisema zao la mwani ni rasilimali muhimu visiwani humo hivyo aliwataka wananchi kuwa na utaratibu wa kutumia bidhaa zinazotokana na zao hilo katika matumizi ya kila siku ili kuongeza thamani ya zao hilo kwa wakulima na serikali kwa ujumla.

Fatma Machalila mkulima wa mwani mkoani Lindi, alisema kutokana na ziara hiyo amejifunza mambo mengi ikiwamo matumizi ya mashine za usarifu wa mwani pamoja na kuona aina za mwani zinazolimwa visiwani Zanzibar.

Hivyo, alizishauri taasisi husika kuwapeleka wakulima wa mwani wa Zanzibar katika maeneo ya Tanzania Bara ambayo yanalimwa zao hilo ili kupeana uzoefu juu ya kilimo hicho.

## Wizara ya Maji kusambaza maji kwa gari

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaaban Ali Othman, amesema wizara hiyo kupitia taasisi yake Mamlaka ya Maji (ZAWA), watahakikisha wanasambaza huduma ya majisafi na salama kwa njia ya gari katika maeneo ambayo wananchi wamekosa huduma hiyo.

Kauli hiyo imekuja kufuatia malalamiko ya baadhi ya wananchi kulalamikia ukosefu wa huduma hiyo tangu kuanza kwa ujenzi wa Mradi wa Barabara ya Mnazi Mmoja hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Unguja. Akizungumza katika ziara maalumu, Othman alisema katika kipindi hiki atahakikisha ZAWA wanawafikishia wananchi huduma hiyo kwa njia ya gari la maji bila ya kuwatoza fedha.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema ukosefu wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo hayo umetokana na kuathirika kwa miundombinu ya maji wakati mradi wa barabara ukiendelea.

Alisema wizara yake imekubaliana na Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi kupitisha mabomba ya maji pembezoni mwa barabara hivyo, muda siyo mrefu mradi huo utakamilika na huduma ya maji itarudishwa kwa wananchi kama kawaida.

Aidha, aliwaomba radhi wananchi waliokosa huduma ya majisafi na salama katika kipindi hiki na serikali imejikita katika kuwaletea maendeleo wananchi wake hivyo barabara ni muhimu na maji ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi, Khadija Khamis Rajab, alisema wizara yake inafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Maji, Nishati na Madini, hivyo watahakikisha wanarudisha miundombinu ya maji na umeme yote iliyoathirika wakati wa ujenzi wa barabara.

Wananchi wanaokosa huduma hiyo ya maji akiwemo Luluwa Salum Ali mkazi wa Kilimani alisema ujenzi wa barabara utakapo kamilika warudishiwe huduma hiyo kwa sababu wanalazimika kununua gari la maji kwa Sh. 15,000 kwa kujaziwa tangi la lita 1,500.

# CHADEMA, Sauti ya Watanzania watoa msimamo zuio mkutano

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Sauti ya Watanzania, vimeendelea na msimamo wao wa kufanya mkutano wa hadhara licha ya ushauri wa Msajili wa Vyama vya Siasa kuwataka wasitishe mkutano huo.

Jana viongozi hao na wananchi mbalimbali walionekana katika viwanja vya Bulyaga, Temeke, jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kushiriki mkutano huo unaoleta pamoja viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa, dini na asasi za kiraia.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alipohojiwa na Nipashe kuhusu msimamo huo, alisema; "Msajili ameshauri tumepokea ushauri wake, lakini sisi tunaendelea na mkutano kama kawaida, watu wanaendelea kumiminika uwanjani hadi sasa."

Juzi Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini imewaita ofisini kwake viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kujadili kuhusu mkutano uliokuwa ufanyike jana na masuala mengine ya utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Msajili alikionya CHADEMA kwa ukiukwaji wa sheria kwa kuwaalika viongozi wa dini wakiwa wamevaa nguo rasmi za taasisi zao za dini na watu wengine ambao siyo wanachama wa chama hicho.

Juzi ofisi hiyo iliwasihi CHADEMA kusitisha mkutano huo uliokuwa umepangwa kufanyika wilayani Temeke, kwa madai ya kuwapo kwa viashiria vya ukiukwaji wa sheria.

"Msajili wa Vyama vya Siasa akiwa ndiye mwenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa yenye masharti yanayokataza masuala hayo na akiwa ni mlezi wa vyama vya siasa, anawasihi CHADEMA msitishe mkutano huo na viongozi wenu wakuu kufika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa tarehe 24, 2023 saa nne asubuhi kuonana naye, ili kuongea," ilisema taarifa ya Msajili Sisty Lyahoza.

Taarifa ilisema imepata taarifa kupitia vyombo vya habari kuwa chama hicho kingefanya mkutano wa hadhara jana na kuwa kimewaalika viongozi wa dini na taaisi zingine, ikiwamo Rais wa Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (TLS), kinyume na sheria za nchi.

Katika taarifa hiyo Sisty, alisema sheria za nchi zinakataza vyama vya siasa kuwa na udini au kutumia dini kufikia malengo yake ya kisiasa pamoja na sheria inayokataza taasisi za dini kufanya shughuli za kisiasa.

Alisema hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko ndani na nje ya nchi kwa watu kudhani kuwa watakachoongea na viongozi hao wa dini na taasisi nyingine katika mkutano huo ni msimamo wa taasisi zao au taasisi zao kuunga mkono kilichoongelewa na chama hicho.

UVAMIZI WA WAANDISHI

Kwa mujibu wa Taarifa kwa Umma iliyotolewa na Bodi ya Uongozi ya Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA Tanzania), tukio hilo linapaswa kulaaniwa na kila Mtanzania au binadamu anayependa ustawi wa taaluma ya habari kwa lengo la kuelimisha, kuburudisha na kukosoa kwa kuwa kuruhusu mashambuzi kama hayo ni kudidimiza na kunyima haki ya msingi kwa Watanzania kupata habari.

Taarifa hiyo ilisema MISA Tanzania ambayo ni taasisi inayopigania uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa inakemea na kulaani vikali tukio hilo na mengine kama hayo. Ni muhimu vyama vya siasa vikaelimisha wafuasi wao dhidi ya mashambulio haya ambayo ni kinyume cha sheria na kuharibu taswira ya nchi.

Taasisi hiyo imeliomba Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kuchunguza kwa kina tukio hilo na kuchukua hatua kali, ikiwamo kuwafikisha mahakamani wote waliohusika na kuwajeruhi, kupora na kuharibu mali za waandishi na dereva wa kampuni hiyo.

Aidha, MISA Tanzania inawaomba Watanzania hususan vijana kuwa walinzi wa kwanza wa amani ya nchi na kuepuka kutumika kufanya vurugu kwenye mikutano au maeneo yoyote nchini kwa kuwa kila mmoja ana uhuru wa kujieleza kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Watanzania ya mwaka 1977.

Wakati huo huo, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umelaani vikali kitendo cha kushambuliwa kwa waandishi wa habari.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Huduma za Utetezi kwa Watetezi wa Haki za Binadamu wa mtandao huo, Wakili, Paul Kisabo alisema; "Kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 waandishi wa habari wana haki na uhuru wa kukusanya taarifa ikiwa ni pamoja na kuuhabarisha umma juu ya taarifa hizo, hivyo kwa namna yoyote ile ni makosa na ni kinyume cha Katiba na sheria za nchi kuwashambulia waandishi wa habari wakiwa wanatekeleza majukumu yao," ilisema.

# Kinana: Rais Samia ni msikivu, nchi imetulia

**Na Mwandishi Wetu, KONDOA**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahaman Kinana, amesema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa ndani ya kipindi cha miaka miwili kutokana na uongozi wake mzuri unaotokana utulivu, usikivu, kupokea ushauri na kufanya uamuzi wa busara kwa manufaa ya Watanzania.

Kinana alitoa kauli hiyo jana wilayani Kondoa mkoani Dodoma katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Kondoa, Dk. Ashatu Kijaji, kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha miaka miwili na nusu chini ya uongozi wa Rais Samia.

"Kwa hali ilivyo na kwa hatua tuliyopiga, tukienda hivi tunavyokwenda mpaka kufika 2025, mimi nina uhakika kila Mtanzania atakuwa na sababu ya kusema tuendelee na CCM, tuendelee na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hatutokuwa na sababu nyingine yoyote, kwanza ni utamaduni wetu CCM hatubadilishi uongozi katikati ya safari. Ukitaka kubadilisha sababu itakuwa nini, hakuna.

"Lazima tumpe mtu nafasi yale aliyokusudia chini ya uongozi wa chama chetu yatimie. Ikifika 2025 tunakwenda na Rais Samia na Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa, amesema kila eneo, kila kata, kila mtaa kila jimbo yako ya kusemea mema, hatuahidi miujiza lakini tumeahidi na yale tuliyoahidi tumeyatekeleza kwa ufanisi mkubwa sana," alisema.



Kinana aliongeza kuwa hawasemi hayo kwa kujivuna, bali kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kulinganisha na hali ya nchi jirani.

Alisema nchi imetulia, ina amani, ina umoja, ina mshikamano, ina malengo na ina mipango ambayo inatekelezwa na kila mtu ni shahidi.

Alisema kuna watu wamejaribu kuigawa kwa misingi ya udini wameshindwa. Kuna waliojaribu kuigawa kwa misingi ya ukabila wameshindwa. Kuna waliojaribu kuigawa kwa misingi ya ubara na visiwani nao wameshindwa.

"Sababu ni misingi imara iliyojengwa na waasisi wa taifa letu, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na marehemu Abeid Aman Karume, misingi yenyewe migumu na mnakumbuka katika kipindi mbalimbali Muungano wetu umepitia kashikashi lakini tumeendelea kuwa imara," alisema.

Pamoja na hayo, Kinana alisema anaungana na wananchi wote na viongozi kumpongeza Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia kwa uongozi wake madhubuti.

"Wakati mwingine baadhi ya watu wanaona kama vile labda tunamsifu sana ndugu Rais lakini hatumsifu kwa mambo ambayo hayana uhakika? Kama nilivyosema ushahidi upo.

Awali akielezea utekelezaji wa Ilani katika Jimbo la Kondoa Vijijini, Dk. Kijaji alimpongeza Rais Samia kwa kuitazama kwa karibu Kondoa ambapo katika kipindi cha miaka miwili na nusu miradi ya maendeleo imepelekwa katika sekta mbalimbali na hiyo ni kutekeleza ahadi za CCM kupitia Ilani ya uchaguzi.

Wabunge na Wajumbe wa Halmashauri ya Taifa (NEC) waliopata nafasi ya kuzungumza katika mkutano huo, wameeleza kwa kina hatua ambazo zinachukuliwa na serikali katika kuboresha sekta ya bandari nchini huku wakitoa rai kwa wananchi kutosikiliza maneno waliyodai ya upotoshaji yanayotolewa na baadhi ya watu.

## STEP inavyobadilisha maisha ya wanaoishi jirani na hifadhi

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Kusimamia Uhifadhi wa Tembo wa Kusini (STEP), kupitia wadau mbalimbali wakiwamo Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) chini ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, imetoa zaidi ya Sh. milioni saba kwa vikundi 12 vya kukopeshana katika Kata ya Mang'ula Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro.

Lengo ni kuviwezesha kiuchumi na kuona faida ya kuhifadhi wanyamapori kupitia miradi ya ufugaji nyuki na ufukuzaji tembo kwenye mashamba ya wananchi.

Mradi huo unatekelezwa katika shoroba ya Udzungwa, Nyerere hadi Selous. Ni wa kwanza wa kisasa Tanzania utakaojengwa kwa umeme, ili kulazimisha wanyama kupita eneo moja na kutoharibu mazao ya wananchi.

Mratibu wa Mradi wa kuboresha uhusiano kati ya tembo na watu wa STEP, Kim Lim akizungumza na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), alisema lengo kuu ni kupunguza uharibifu wa mazao unaosababishwa na wanyama pamoja na kuwezesha jamii kuongeza kipato na kutoa elimu kwa wanafunzi.

"Kwenye VIKOBA tunafanya kazi na vikundi 12 vyenye jumla ya wanachama 250 ambao asilimia 50 ni wanawake na vijana, tangu mwaka 2020 hadi sasa tumeona vinawasaidia sana kutatua changamoto za maisha yao," alisema. Kwa mujibu wa Kim, mikopo iliyotolewa ni zaidi ya Sh. milioni saba na wanakikundi walinunua hisa zenye thamani ya Sh. milioni 35, kwamba kila wakinunua wanatumia kuchukua mikopo kwa ajili ya shughuli za kilimo na kurejesha.

Mtaalamu wa Nyuki wa Kikundi cha NJOKOMONI, Ahemed Churi, alisema tembo walikuwa kero hali iliyosababisha wakulima kushindwa kulima ndipo walipokuja na mradi wa kuzuia tembo mwaka 2012 na STEP iliwafundisha kutengeneza uzio wa pilipili kwa kuweka vitambaa ambavyo akinusa anapiga chafya na kurudi, lakini baadaye wakigundua wakaanza kugeuka kinyumenyume na kuingia shambani.

"Tukabuni mradi wa nyuki kwamba ukiweka mizinga tembo hawataingia, kwa ufadhili wa Hifadhi ya Taifa Udzungwa tulipata mizinga 20 na baadaye STEP wakatupa mizinga 100 ambayo tumeiweka umbali wa mita moja, iliyounganishwa na nyaya ambayo tembo akija akitikisa nyuki wanatoka na kung'ata, anakimbia," anasema.

Aidha, anasema mradi huo kwenye eneo la kilomita moja na mizinga 76 na yenye nyuki ni 19 pekee umekuwa na manufaa kwa kuwa zamani tembo walikuwa wanaingia katika mashamba lakini sasa mradi una faida kwa asilimia 99.6, tembo kuingia kwa jamii ni nadra na tunapata mazao ya nyuki.

"Nyakati za nyumba tulikuwa tunaopata hadi lita 55, ilijitokeza changamoto ya sisimizi kuingia kwenye mizinga tukapata suluhisho la kuweka vifuniko vya soda, ikajitokeza nyingine ya mdudu nyegere anafunua mzingira lakini tuliwawinda na walikimbia," anasema.

HABARI KIMATAIFA

## Watu 16 wauawa Darfur shambulio la roketi

**DARFUR,** SUDAN

CHAMA cha Wanasheria katika Mkoa wa Darfur kimesema watu 16 wameuawa kwa shambulizi la roketi ambalo limepiga nyumba zao katika mkoa huo, magharibi mwa Sudan wakati wa majibizano ya roketi kati ya jeshi na wanamgambo wa msaada wa haraka (RSF).

Eneo hilo kubwa ambalo tayari limeharibiwa na vita vya kikatili mwanzoni mwa miaka ya 2,000 limeshuhudia baadhi ya ghasia mbaya sana tangu mapigano yalipozuka katikati ya mwezi Aprili kati ya majenerali wanaohasimiana wa Sudan wanaowania madaraka.

Mbali na mauaji hayo, watu wameendelea kuyakimbia makazi yao, wakati huu maelfu wakikimbilia katika nchi jirani ya Chad kutokana na vita hivyo ambavyo vimesababisha vifo vya watu 3000, kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa (UN).

Inaelezwa kuwa mapigano yanayoendelea, yamekuwa yakilenga zaidi katika mji wa El Geneina, ambako UN umeripoti mauaji makubwa ya raia, pamoja na visa vingine vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mauaji hayo yanakuja siku chache baada ya kiongozi wa mashtaka kwenye Mahakama ya Kimataifa ya (ICC) Karim Khan kutangaza kuwa ofisi yake inachunguza ripoti ya kutokea kwa uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur, baada ya miili ya watu 87 kutoka kabila la Masalit kukutwa katika kaburi la pamoja. **RFI**

## Wananchi Botswana waandamana kupinga mswaada wa ushoga

**GABORONE,** BOTSWANA

MAMIA ya watu wameingia mitaani katika mji mkuu wa Gaborone nchini Botswana kupinga mswaada unaotaka kuhalalisha mahusiano ya jinsia moja.

Maandamano hayo yaliyoungwa mkono na makundi ya kidini, yalifanyika mji mzima kuelezea upinzani wao kwa mswaada ambao una lengo la kutekeleza maamuzi ya mahakama mwaka 2019 yanayounga mkono haki za wanaojihusisha na ushoga.

Inaelezwa kuwa baadhi ya wananchi walishika mabango yanayosomeka

"Tunasema hapana kwa ushoga" na "Tuwalinde watoto wetu".

Mchungaji Pulafela Siele wa ushirika wa ki-injili wa Botswana, alisema mswaada huo utafungua milango ya uasherati na upotoshaji. Tunalisihi bunge letu lichague kura ya maoni kuhusu suala hili. **VOA**

# Putin: Mashambulizi ya Ukraine yamekwama

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema mashambulizi ya Ukraine kwa Russia yamekwama na kwamba ameyasema hayo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na mwenzake wa Belarus, Alexander Lukashenko.

Ilielezwa kuwa wawili hao walikutana jana mjini St. Petersburg, na kwamba katika mazungumzo hayo ya siku mbili watazungumzia masuala ya usalama mashariki mwa Ulaya.

Russia na Belarus ni washirika wa muda mrefu katika uhusiano ambao Moscow ndiyo inayotawala sehemu kubwa ya ushirika huo, ikielezwa kuwa Lukashenko amekuwa akionesha umuhimu wake kwa Putin tangu majeshi ya nchi hiyo yalipoivamia Ukraine Februari 2022 ambako aliruhusu Belarus itumike kama sehemu ya kufanikisha mashambulizi mwanzoni mwa vita.

Aliruhusu majeshi ya Moscow yafanye mafunzo katika ngome zake za kijeshi na kwamba mafunzo hayo mara nyingi yalihusisha mazoezi ya pamoja ya kijeshi huku alipokea silaha za kimkakati za nyuklia ambazo Putin amezipeleka Belarus, hatua iliyolaaniwa vikali na mataifa ya magharibi.

Ikulu ya Kremlin ilimpongeza pia Lukashenko kwa kusimamia makubaliano ya mwezi uliopita ya kuzima uasi wa wapiganaji wa Wagner ambao Putin anasema kwa muda mfupi, ulitishia kuiingiza Russia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Lukashenko hajatoa ahadi ya kupeleka jeshi lake dogo liungane na Moscow katika vita, lakini hatari ya mashambulizi mapya kutoka katika ardhi ya Belarus inaisukuma Ukraine kulinda mpaka wake wa upande wa kaskazini.

Aidha, ilielezwa kuwa Russia iliushambulia tena mji wa bandari ya Bahari Nyeusi wa Odesa nchini Ukraine, taarifa iliyotolewa na maofisa wa Ukraine wakati Russia ikiendeleza mashambulizi ambayo yameharibu miundombinu muhimu ya bandari kusini mwa Ukraine wiki moja iliyopita.

Ilielezwa kuwa mashambulizi hayo yamesababisha kifo cha mtu mmoja, watu wengine 22 wakijeruhiwa kwenye tukio hilo lililosambaratisha pia kanisa ambalo ni alama muhimu ya dhehebu la Orthodox kwenye mji huo.

Gavana wa eneo hilo Oleh Kiper, alisema watoto wanne ni kati ya waliojeruhiwa katika mlipuko uliotokana na shambulio hilo, Kiper akieleza kuwa, majengo sita ya makazi ya watu nayo yameharibiwa.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa Russia imekuwa ikifanya mashambulizi mfululizo kuilenga Odesa , mji ambao ni kituo muhimu cha kusafirisha nafaka tangu Moscow ilipojitoa katika mkataba wa usafirishaji wa bidhaa za kilimo licha ya juhudi za Kyiv kutaka kurejesha maeneo yake yaliyonyakuliwa. **DW**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, alipowasili kwenye mgahawa akiwa na Mbunge mpya wa Conservative, Steve Tuckwell, jana. **PICHA: AFP**

# UN yalaani marufuku ya wanawake kusafiri peke yao

**TRIPOLI,** LIBYA

WATAALAMU wa Umoja wa Mataifa (UN) wamelaani sera ya serikali ya Libya ya kuwazuia wanawake kusafiri nje ya nchi bila kuandamana na mwanamume.

Hatua hiyo ilipitishwa takriban miezi mitatu iliyopita na serikali ya Abdel Dbeibah, yenye makao yake mjini Tripoli na ambayo inashiriki madaraka na serikali sambamba, iliyoko mashariki mwa Libya.

Sheria hiyo mpya, iliyochukuliwa dhahiri chini ya shinikizo kutoka kwa wanamgambo wa Kiislam wenye msimamo mkali wa dini huko Tripoli, inawalazimisha wanawake na wasichana kuwa na mwanamume, anayeitwa mahram, ili waweze kusafiri na kujaza fomu ya kina inayobainisha sababu za safari yao, na kwamba wanaokataa wamepigwa marufuku kuondoka nchini Libya.

Ilielezwa kuwa serikali ya Dbeibah ilitakiwa kutoa maelezo kwa wataalamu wa UN kuhusu hatua hiyo, lakini, baada ya siku 60, wataalamu hao walishutumu hadharani sera hiyo ya kibaguzi dhidi ya

wanawake na ambayo inapinga haki za kimsingi na uhuru wa wanawake na wasichana.

Wataalamu hao wa UN pia wamezitaka mamlaka za Libya kukomesha aina zote za unyanyasaji, ubaguzi na mashambulizi yanayofanywa na vyombo vya usalama dhidi ya wanawake watetezi wa haki za binadamu na wale ambao wamepinga sera hiyo ya kibaguzi katika kipindi cha miezi miwili iliyopita.

"Serikali haina lingine ila kuondoa sheria hii ya kibaguzi, ambayo inakinzana na sheria zote za kitaifa za Libya," alisema Zahara Langui, mkurugenzi mtendaji wa Jukwaa la Wanawake wa Libya kwa ajili ya amani na mwanaharakati wa haki za binadamu.

**VOA**

HABARI MICHEZO

# KAZE KUNOGESHA BENCHI LA UFUNDI NAMUNGO FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, yeye na Klabu ya Namungo mambo ni 'bambam' na muda wowote kuanzia jana alitarajiwa kutangazwa kuwa mkuu wa benchi la ufundi la timu hiyo ya Ruangwa mkoni Lindi.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili zimeeleza kuwa Kaze yuko kwenye mazungumzo na uongozi wa timu hiyo kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye benchi la ufundi ambalo kwa sasa liko chini ya kocha Denis Kitambi.

"Kaze anakuja kuwa kocha mkuu na Kitambi atakuwa msaidizi huku Nsajigwa (Shadrack) akiendelea na majukumu yake ya kocha wa viungo," kilieleza chanzo chetu makini ndani ya klabu hiyo.

Hata hivyo, Nipashe lililazimika kumtafuta Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Suleimani, ili kujua ukweli wa taarifa hizo, ambaye alisema watafanya maboresho kwa kuongeza nguvu katika benchi lao la ufundi na suala hilo linafanyiwa kazi na kamati ya mashindano kulingana na mahitaji ya timu hiyo.

"Timu yetu ipo Karatu chini ya kocha wetu Kitambi akisaidiana na Nsajigwa, ninaimani kutakuwa na maboresho ambayo yanafanywa na kamati husika," alisema Katibu huyo.

Kuhusu Kaze, alisema ni mapema kulizungumzia suala la kocha huyo kwa sababu liko kwenye kamati ya mashindano wanalifanyia kazi ikiwamo suala zima la maboresho ya timu yao katika kila sekta.

Kikosi cha Namungo FC kimeweka kambi Karatu, Arusha na kitacheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Singida Fountain Gate FC, mchezo utakaopigwa leo, mkoani humo.

Kikiwa huko kitacheza mechi mbili za kirafiki kabla ya kurejea Dar es Salaam na kucheza mingine miwili na baada ya hapo kitarudi maskani kwao, Ruangwa, Lindi tayari kwa kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

MAGONGO...



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilala Wanawake wenye jezi za rangi ya machungwa na wanafunzi wa Hockey Queens, wakiwania mpira wakati wa michuano ya saba kwa vijana ya mpira wa magongo iliyofanyika katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania Kriketi, Namibia dimbani

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya vijana ya Tanzania ya mchezo wa Kriketi, inashuka dimbani leo kucheza dhidi ya Namibia kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia kwa wanaume chini ya miaka 19 (ICC U-19), zitakazofanyika mwakani nchini Sri Lanka.

Mchezo huo utachezwa katika viwanja vya Gymkhana na mechi ya pili itakuwa kati ya Sierra Leone dhidi ya Nigeria, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dar-es-Salaam leo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Kriketi Tanzania, Jimmy Kamande, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wachezaji kushika mafunzo mazuri na atatoa uzoefu wake kwa wachezaji ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Alisema anajivunia ubora wa kikosi chake na wachezaji kushika mafunzo aliyowapa vizuri kwa kipindi cha mwezi mmoja na kwamba kucheza mechi za kirafiki kumemsaidia kuona ubora na madhaifu ya timu yake.

"Michezo miwili ya kirafiki imekuwa kipimo bora kwa kikosi chetu kuona ni masuala gani tunatakiwa kuyashughulikia ili kujenga kikosi imara na chenye ushindani, matokeo hayakuwa suala la muhimu kwetu, tulihitaji kuangalia tu kile tunachopaswa kufanya ili kuboresha," alisema Jimmy.

Alisema waliweka kambi kwa takriban mwezi mmoja ili waweze kufanya mazoezi na kupata uwiano kwa sababu ya mashindano hayo makubwa ambayo wamelenga kufuzu.

Tanzania ni wenyeji wa michuano hiyo inayoshirikisha timu sita ikiwamo Kenya, Nigeria, Namibia, Uganda na Sierra Leone.

## Sayari Women, Mwanga City sasa hazishikiki

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Sayari Women ya Dar es Salaam, Mwanga City Queens ya Kigoma, Gets Program ya Dodoma na Mpaju Queens ya Mbeya, zinaongoza msimamo wa makundi Ligi ya Soka Mabingwa Mikoa Wanawake nchini inayoendelea kutimua vumbi jijini Mwanza.

Kwenye michuano hiyo inayochezwa viwanja vya CCM Kirumba na Nyamagana, timu ya Mpaju Queens inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 10, ikicheza mechi nne, ikifuatiwa na Ifakara Home ya Morogoro yenye pointi nane, Mandozi Princess ya Mwanza ambayo ina alama saba, Singida Rising Stars pointi tatu, huku Mwanga FDC ya Shinyanga ikiwa haina pointi.

Kundi B linaongozwa na Mwanga City Queens yenye pointi 10 kwa mechi nne ambazo imecheza, Mara Princess ikiwa na pointi saba, nafasi ya tatu ikichukuliwa na Chipuputa Queens ya Mtwara yenye alama sita, Maendeleo Queens ya Songwe pointi nne na Kilimanjaro Wanderers ya Kilimanjaro ikiwa na alama moja.

Gets Program inaongoza Kundi C ikiwa na pointi 12, nayo ikicheza mechi nne, Ziba Sekondari ya Tabora ya pili ikiwa na pointi tisa, Young Stars Queens ya tatu na pointi zake nne, Raha Queens ya Simiyu pointi nne na inayoshika mkia ni Ilula FDC Queens ya Iringa ambayo haina pointi.

Sayari Women inaliongoza Kundi D ikiwa na pointi saba, Njombe FDC Queens ina pointi tano, Coastal Ladies ya Tanga pointi mbili na Shadow Girls ya Geita ikiwa na pointi moja.

Wachezaji walio orodha ya juu kwenye upachikaji mabao kwenye ligi hiyo ni Mwatima Mwarabu wa Ziba Sekondari mwenye mabao 12, akifungana na Irene Chitanda wa Gets Program ambaye naye pia ana idadi kama hiyo.

Hawa Haji wa Ziba Sekondari ana mabao saba, Shadia Omari wa Young Star Queens na Latifa Athumani wa Chipuputa Queens wana mabao sita kila mmoja, Christa Bella wa Mwanga City Queens, Maria Juvel wa Gets Program, wana mabao matano kila mmoja na Salma Mohamed (Ziba Sekondari), Zawadi Kusekwa (Shadow Girls) na Pili Tandika wa Gets Program kila mmoja akiwa amecheka na nyavu mara nne.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATAKIWA SAUDIA

CHELSEA na Klabu ya Saudia, Al-Hilal, zimeanza mchakato wa kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, ambaye hajasafiri na Paris St-Germain katika ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi huko barani Asia. **(RMC Sport)**

### MBAPPE NA OFA YA MESSI

AL-Hilal wamempa Kylian Mbappe ofa ile ile waliyotoa kwa Lionel Messi ya euro milioni 400 kwa mwaka hadi 2026, ingawa kimsingi ana makubaliano ya kujiunga na Real Madrid kama mchezaji huru msimu ujao wa majira ya joto. **(Nicolo Schira)**

### KANE SAFI BAYERN

MKE wa Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, ameonekana jijini Munich akitafuta nyumba na shule kabla ya uwezekano wa nyota huyo kuhama kutoka Tottenham Hotspur kwenda Bayern Munich. **(Bild)**

### KUDUS AMULIKWA CHELSEA

CHELSEA imefanya mawasiliano na Ajax kuhusu nia yao ya kutaka kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ghana, Mohammed Kudus, 022. **(The Athletic)**

### OSIMHEN NA NAPOLI BADO

MAZUNGUMZO ya mkataba mpya kati ya Victor Osimhen na timu yake ya Napoli bado yamekwama na hivyo kufungua milango kwa Chelsea au Manchester United kujaribu kumsajili mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24. **(Corriere dello Sport, via Goal)**

### LUKAKU BASI TENA INTER

INTER Milan inaamini kuwa sasa haiwezekani kufikiria kumrejesha Romelu Lukaku katika klabu hiyo kutoka Chelsea baada ya mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa 30, kuwasiliana na wapinzani wao, AC Milan na Juventus kuhusu uwezekano wa kuhamia huko. **(Gazzetta dello Sport)**

### ZAHA APEWA OFA

KLABU ya Galatasaray imempa ofa yenye thamani ya euro milioni nane kwa mwaka mshambuliaji wa Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 30, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake pale Crystal Palace kumalizika. **(Mirror)**

### SUAREZ KUMFUATA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 36, yuko tayari kulipa kutoka mfukoni mwake ili kuondoka Gremio na kwenda Klabu ya Inter Miami, kuungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi **(ESPN, via Sport)**

### GVARDIOL NI MILIONI 87

KLABU ya Manchester City wameambiwa watalazimika kulipa thamani ya pauni milioni 87 kwa RB Leipzig ili kumsajili mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, 21. **(Sunday Mirror)**

### LAPORTE ATAKIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumnunua mlinzi wa Manchester City, Aymeric Laporte, 29. **(Star Sunday)**

### WAN-BISSAKA KUONGEZEWA

KLABU ya Manchester United inaonekana kuwa tayari kumwongeza mkataba wa mwaka wa ziada beki wa kulia wa England, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 25, kama kipengele cha mkataba wake kinavyoruhusu, licha ya Palace kutaka kumsajili tena. **(Star Sunday)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AFURAHIA KUIFUNGA ARSENAL

●●●Ni mpinzani mzuri sana, walicheza vizuri sana msimu uliopita kwenye Ligi Kuu, kwa hiyo...

**NEW JERSEY, Marekani**

ERIK ten Hag alifurahishwa na kiwango cha Manchester United cha kumiliki mpira walipoanza ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Arsenal.

Wakiwa wameshinda dhidi ya Leeds United mjini Oslo nchini Norway na Lyon kule Edinburgh, 'Mashetani Wekundu' hao walianza maandalizi ya msimu mpya wa 2023-24 kwenye Uwanja wa MetLife huko New Jersey, Jumamosi.

Nahodha aliyeteuliwa hivi karibuni, Bruno Fernandes, alimshinda kwa urahisi kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale kabla ya Jadon Sancho kufunga kufuatia makosa ya Gabriel katika ushindi huo wa 2-0.

"Nadhani ni nzuri sana," alisema Ten Hag.

"Jinsi tulivyocheza, nilifurahishwa sana, jinsi tulivyokuwa wachangamfu ndani na nje ya kumiliki mpira.

"Hivyo ndivyo tunavyotaka kucheza na hicho ndicho kipindi pekee cha mwaka ambacho unaweza kufanya kazi katika mazoezi na kutafsiri kwa michezo bila matokeo.

"Lakini bado, tunataka kushinda na nadhani vijana walionesha unavyotaka kucheza mchezo mzuri.

"Bila shaka, yote ni michezo mizuri. Tunapaswa kwenda na inatusaidia kupata maendeleo na hasa wale wapinzani, ni wazuri.

"Arsenal ni mpinzani mzuri sana. Walicheza vizuri sana msimu uliopita kwenye Ligi Kuu, kwa hiyo ni vizuri kulinganishwa nao, basi utakuwa msimu bora zaidi."

Jambo kuu hasi lilikuwa jeraha la kipindi cha pili kwa Amad Diallo, ambaye aliondoka Uwanja wa MetLife kwa magongo huku mguu wake wa kushoto ukiwa umefungwa kamba.

Ten Hag anatumai kuwa kinda huyo ameepuka jeraha la aina yoyote usiku ambapo kiungo wa kati Kobbie Mainoo mwenye umri wa miaka 18, alicheza vizuri.

"Inapendeza," alisema Mholanzi huyo akiiambia MUTV.

"Manchester United inasifika kwa kuwalea wachezaji wachanga kila mara na inaweza kufanyika. Lakini tunapaswa kuona.

"Tunajiamini, anacheza kwa kujiamini na anapenda sana uchezaji wake. Lakini mwaka huu, aliionesha katika chemchemi, kisha akajeruhiwa. Tuna furaha kweli."

# CHELSEA YAJITOSA KWA KUDUS




**LONDON, England**

CHELSEA wamefanya mazungumzo ya kutaka kumnunua kiungo mshambuliaji wa Ajax, Mohammed Kudus.

Arsenal na Brighton pia wameonesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 40 baada ya kukataa ofa ya kuongeza mkataba mpya.

Kudus, ambaye nusura ajiunge na Everton mwaka mmoja uliopita, alivutia kwenye Kombe la Dunia 2022 akiwa na Ghana.

Hili linakuja wakati kikosi hicho cha Mauricio Pochettino kikiwa kwenye mvutano na Brighton kuhusu kupatikana kwa nyota wa pauni milioni 100, Moises Caicedo, huku kocha Roberto De Zerbi akionesha wazi msimamo wake thabiti wa kutomruhusu raia huyo wa Ecuador kuondoka.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ghana alinyakuliwa na klabu hiyo ya Eredivisie mwaka 2020 kwa pauni milioni nane baada ya kuonesha kiwango kizuri katika klabu yake ya zamani ya FC Nordsjaelland.

Alianza maisha polepole pale Amsterdam, akijitahidi kusisitiza nafasi yake kwenye timu nyuma ya Anthony, ambaye aliondoka kwenda Manchester United mnamo mwaka 2022.

Kwa mujibu wa The Athletic, 'The Blues' wanakaribia kukubaliana na maslahi binafsi na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ghana.

Kudus alikuwa wa pili kwa ubora katika msururu wa mabao, lakini baada ya Mbrazil huyo kuondoka, alifanikiwa katika klabu hiyo ya Uholanzi, akifunga mara 11 katika mechi 30 za ligi msimu uliopita.

Alikuwa muhimu kwa Ajax wakati wa mbio zao za Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka jana, akifunga katika mechi nne kati ya sita za mashindano hayo, haswa akifunga dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield.

Uchezaji mzuri wa nyota huyo wa kutumainiwa umevutia hisia za klabu nyingi za Ligi Kuu England.

Erik ten Hag pia alikuwa anatazamia kutaka kumnunua kiungo wake huyo wa zamani, kabla ya United kumsajili Mason Mount.

Arsenal na Brighton ndizo klabu zilizopo kwenye foleni inayokua ya mahali ambapo mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ghana anahitajika.

# Aston Villa wamsajili Diaby

**LONDON, England**

KLABU ya Aston Villa imekamilisha usajili wa winga, Moussa Diaby, kutoka Bayer Leverkusen kwa ada iliyovunja rekodi ya klabu.

Miamba wa Saudi Arabia Al Nassr pia walivutiwa na Diaby na wakaingia kwenye vita vya kutaka kumgombea na Villa, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alikataa kuhamia Mashariki ya Kati ili kuungana na Unai Emery katika Villa Park.

Mkataba huo sasa umekamilika na tayari Diaby amesafiri kwenda Marekani kuungana na timu yake mpya kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Villa wanadaiwa kutenga zaidi ya pauni milioni 50 ili kumsajili Diaby, ambaye anakuwa rekodi mpya ya usajili wa Villa.

Diaby anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na Villa msimu huu wa majira ya joto, kiungo Youri Tielemans na beki wa kati Pau Torres, kuhamia West Midlands.

Diaby, winga wa kulia kwa asili, alifurahia msimu mzuri zaidi wa kazi yake mwaka jana.

Kwenye mechi 48 katika michuano yote, Mfaransa huyo alipachika mabao 14 na kutoa 'asisti' za mabao 11.

Kutakuwa na muunganiko pale Villa Park kwa Diaby na winga mwenzake Leon Bailey, ambaye aliondoka Leverkusen miaka ishirini iliyopita.




# Guardiola hajui kikosi chake kitavyokuwa

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amekiri kwamba hajui jinsi kikosi cha Manchester City kitakavyokuwa wakati wa kuanza kutetea mataji yake matatu msimu huu.

Guardiola amezungumza na Kyle Walker huku kukiwa na nia ya kutoka kwa Bayern Munich, lakini beki huyo bado hajaamua juu ya mustakabali wake, wakati Bernardo Silva na Aymeric Laporte wote wanaweza kuondoka.

Hali ya kutokuwa shwari pale City ni wasiwasi kwa Guardiola, aliyepewa jukumu la kuipa historia tena timu hiyo.

"Tutaona tulichonacho mwisho wa dirisha la uhamisho, tutakuwa na timu gani," alisema Guardiola.

"Kusema kweli sikufikiria kuwa kutakuwa na harakati hii. Mambo mengi yanaenda kutokea. Ndio maana siwezi kujibu kwa sababu sijui.

"Nawatakia mema wachezaji wangu na bila shaka klabu inahusika na hilo pia. Nilizungumza na Kyle na kila kitu kiko sawa. Tutaona kitakachotokea. Siwezi kusema lolote kwa sababu bado nafikiria hilo."

City wamemlenga beki wa kati wa Croatia, Josko Gvardiol, lakini hawajafikia thamani ya RB Leipzig, inayodhaniwa kuwa zaidi ya pauni milioni 80 na hadi sasa wamemnunua Mateo Kovacic pekee kutoka Chelsea kwa pauni milioni 25.

Riyad Mahrez anamfuata Ilkay Gundogan nje ya mlango, huku winga huyo akipata uhamisho wa pauni milioni 30 kwenda Al-Ahli, huku Joao Cancelo akirejea baada ya mzozo kati yake na Guardiola uliosababisha akopeshwe kwa Bayern Januari.

"Joao amekuwa muhimu sana kwetu siku za nyuma," alisema Guardiola.

HABARI MICHEZO

# WAZIRI MKUU AKOSHWA UWEKEZAJI NBC KUKUZA SEKTA YA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Benki ya NBC kwa kuwa chachu ya kuendeleza sekta ya michezo nchini huku akizitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa benki hiyo.

Akizungumza wakati wa hitimisho la mbio za NBC Dodoma Marathon 2023 zilizofanyika jijini Dodoma jana, Majaliwa alisema pamoja na mbio hizo ambazo benki hiyo imeandaa kwa mwaka wanne mfululizo, benki hiyo pia ni mdhamini mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Watanzania mnajua, benki hii ndio mdhamini mkuu wa Ligi Kuu yetu ya Tanzania yaani NBC Premier League, ambayo ni ligi maarufu barani Afrika kwa sasa. Hii ni kutokana na jitihda za Benki ya NBC," alisema.

Majaliwa alisema uwekezaji wa benki hiyo katika Ligi Kuu umekuwa na tija kubwa na kuipaisha ligi hiyo kimataifa katika miaka ya hivi karibuni.

Kuhusu NBC Marathon 2023, Majaliwa alisema: "Jambo hili la NBC Marathon 2023 linalofanyika hapa leo ni kubwa sana na sisi kama washiriki, tumefarijika sana. Naishukuru benki hii na naamini jitihada zake zitasaidia kuimarisha afya ya mama na mtoto na mbio hizi zimeendelea kupata umaarufu hapa nchini na kimataifa kwa ujumla."

Majaliwa alisema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zote za kuboresha michezo kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi ikiwamo NBC.

"Ni ukweli usiopingika kuwa Benki ya NBC imekuwa miongoni mwa wadau muhimu sana katika maendeleo ya sekta ya michezo nchini. Naipongeza benki hii kwa kuunga mkono jitihada za Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan za kuwekeza katika michezo. Sisi kama serikali, tunatambua kuwa michezo imekuwa ajira na uwezeshaji," alisema.

Alisema matunda ya uwekezaji wa benki hiyo hasa katika Ligi Kuu yameanza kuonekana kutokana na kupanda kwa thamani ya wanamichezo hata katika michezo mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu, riadha na muziki.

"Sekta ya sanaa na michezo imekuwa ikitoa mchango mkubwa siyo tu kiafya kwa Watanzania, lakini pia ajira na hasa kwa vijana.

Mbio za NBC Marathon 2023, zilikutanisha wanariadha zaidi ya elfu tano kutoka mikoa mbalimbali nchini huku washindi katika kilometa 42, 21, 10 na tano wakiondoka na zawadi nono za fedha.

Katika mbio za kilometa 10, Mraaco Monco aliibuka mshindi wa kwanza na kujishindia kitita cha shilingi milioni 2 baada ya kutumia dakika 32 na sekunde 25.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akipasha misuli kabla ya kushiriki katika mbio za NBC Dodoma Marathon, zilizofanyika katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma jana. Kushoto kwake ni Waziri wa Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana na kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibabage atabiri makubwa Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

BEKI wa pembeni wa Klabu ya Yanga, Nickson Kibabage, amesema anaamini kama wakishirikiana vizuri na wachezaji wenzake kikosini, wanaweza kuipa mafanikio makubwa timu hiyo ambayo msimu ujao itakuwa na kazi kubwa ya kutetea mataji yake na kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe juzi usiku baada ya kumalizika kwa mchezo wa kirafiki wa Kimataifa dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye Kilele cha Siku ya Mwananchi, alisema mashabiki wa Yanga wasubiri kuona ushindani mkubwa msimu ujao.

"Nitatumia uwezo wangu kuhakikisha msimu ujao ninashirikiana na wachezaji wenzangu kutetea makombe yetu yote," alisema Kibabage, ambaye ni mchezaji mpya katika kikosi hicho.

Alisema anashukuru ushirikiano anaopewa na wachezaji wenzake kikosini tangu alipoungana nao mpaka sasa.

Akizungumzia mchezo wao huo, alisema ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa na kudai utawasaidia kufanya vizuri katika mechi zilizopo mbele yao.

"Mchezo ulikuwa mzuri, kila mchezaji aliweza kuonesha kiwango chake, kwa upande wangu ninazidi kujifunza vitu vingi ambavyo vitanisaidia siku zijazo," alisema.

Aidha, alisema malengo yake ni kucheza soka la kulipwa nje ya nchi ili atimize malengo aliyojiwekea.

## Gamondi atoa uchambuzi

INATOKA UK. 24

sha lao kwa kusherehekea Kilele cha Siku ya Mwananchi na kutambulisha nyota 26 ambao watakuwapo kwenye kikosi cha timu hiyo kwa msimu wa 2023/24.

Katika utambulisho huo, Yannick Bangala, Djuma Shaaban na Mamadou Doumbia hawakuwapo kwenye orodha pamoja na Fiston Mayele, ambaye inaelezwa tayari ametimkia kunako Klabu ya Pyramids ya Misri.

"Kuhusu 'THANK YOU', hili itaendelea baada ya kamati itakapokutana na kufanya tathmini pamoja na kuweka wazi hatima ya wachezaji wetu wengine," alisema Kamwe.

## Simba yashusha kipa 'tall' Mbrazili

INATOKA UK. 24

"Jefferson ana uwezo mkubwa wa kulinda lango huku akitumia miguu yote miwili kwa ufasaha na kumudu kuanzisha mashambulizi pia akiwa na uzoefu wa kucheza mechi nyingi za ushindani."

Kipa huyo mwenye uzito wa kilo 84 na urefu wa sentimeta 192 (mita 1.92), anaonekana kuja kuleta chachu kwenye eneo la golikipa ambalo tangu mwaka 2017, lilikuwa chini ya himaya ya Manula.

Hata hivyo, hakuna shabiki yeyote wa soka nchini wakiwamo wanachama na wapenzi wa Simba waliotegemea kusajiliwa kipa huyu, badala yake wengi walidhani atakuwa mmoja wa wale wawili ambao walitajwa sana kwenye tetesi, akiwamo Mbrazil Caique Luiz Santos na Simon Omossola raia wa Cameroon anayeichezea FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Awali, taarifa za ndani ya klabu zilibainisha kuwa Simba waliachana na Mbazil Caique kwa sababu hajui lugha ya Kingereza wala Kifaransa, badala yake anafahamu Kireno kitu ambacho kiliwafanya mabosi wa klabu kuwa na wasiwasi jinsi atakavyokuwa akiwasiliana na mabeki wa timu hiyo wanaofahamu zaidi lugha za Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili.

Taarifa zilizidi kudai kuwa viongozi wa Simba waliangukia kwa Omossola na tayari walishaanza mazungumzo, lakini Kocha Mkuu, Mbazili Robertinho Oliveira, alikatisha dili hilo kwani aliwaambia anataka kipa kutoka Brazil na si vinginevyo.

"Alituambia anataka kipa kutoka Brazil tu kwa gharama yoyote ile, kwa hiyo ikaanza kazi nyingine ya kumsaka kipa bora na ambaye atafahamu angalau lugha ya Kiingereza, tumempata huyu kwa msaada wake pia, ni kipa mzuri sana," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo.

Kusajiliwa kwa kipa huyo na Luis Miquissone kunafanya timu hiyo kuwa na wachezaji 14 wa kigeni, hivyo ni lazima wawili wakatwe ili kukidhi kanuni ya Ligi Kuu Bara.

Lakini Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wanachofanya kwanza ni kusajili kila mchezaji ambaye wanamhitaji na baadaye ndipo watakaa kuangalia nani ampishe nani.

# Michezo

Jumatatu Julai 24, 2023

Nipashe




## Ten Hag afurahia kuifunga Arsenal

UKURASA 21

# GAMONDI ATOA UCHAMBUZI WA KIKOSI YANGA

●●●Ni baada ya Kaizer Chiefs kumwonyesha mwanga, uongozi wafunguka kuhusu Bangala...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuiongoza timu yake katika mechi ya kwanza ya kirafiki kwa mara ya kwanza tangu aanze kuinoa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Angel Gamondi, ameeleza kufurahishwa na kiwango kizuri kilichooneshwa na wachezaji kwenye mchezo huo dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, ukiwa maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wao kwenye Kilele cha Siku ya Mwananchi, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0, likifungwa na Kennedy Musonda baada ya pasi murua kutoka kwa Max Pia Nzengeli.



Gamondi

Baada ya kukamilika kwa dakika 90, Gamondi alisema alichoangalia zaidi ni muungano wa wachezaji wake na matokeo ilikuwa si muhimu sana kwake kwa sababu hakuwa na muda mrefu wa kufanya maandalizi.

Alisema alikuwa na siku 10 za maandalizi kwa sababu ya kuchelewa kujiunga kwa wachezaji wapya kutokana na usajili wa nyota hao kuchelewa.

"Hatukuwa na muda mrefu kwenye maandalizi, lakini nafurahi kuona wachezaji wamekuwa na muunganiko mzuri, tumetengeneza nafasi tatu tumekosa na kupata moja na kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

"Mechi hii ni kipimo kizuri kwangu kwa kuwa nimeona ubora na madhaifu ya timu yangu, wapi natakiwa kufanya kazi, ilikuwa mechi nzuri ya mbinu na ufundi kwa kila timu," alisema Gamondi.

Kuhusu wachezaji wapya, alisema ameona muunganiko mzuri wa nyota hao na waliokuwapo tangu awali kwa kuonesha soka la kuvutia licha ya kwamba bado kuna mapungufu anatakiwa kuyafanyia kazi kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Naye Kocha Mkuu wa Kaizer Chiefs, Molefi Ntseki, alisema mechi hiyo ilikuwa kipimo kizuri kwa timu zote mbili, kiufundi na mbinu na kila mmoja amenufaika.

Alisema timu zote zilicheza vizuri na ameona mapungufu ya kikosi chake hivyo anakwenda kuyafanyia kazi kwa sababu amepata kipimo kizuri cha maandalizi ya msimu mpya.

"Japo wamepoteza, lakini nimefurahi kupata mechi dhidi ya Yanga ambayo imenipa mwanga wa mapungufu ya kikosi changu na timu zote zimecheza vizuri," alisema kocha huyo.

Katika hatua nyingine, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema hatima ya wachezaji wanne ambao hawakutambulishwa katika Kilele cha Siku ya Mwananchi, wataiweka wazi hivi karibuni.

Yanga juzi walikamilisha tama-

UKURASA. 23




# Simba yashusha kipa 'tall' Mbrazili

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza kwenye historia yake, Klabu ya Simba imemsajili kipa kutoka nchini Brazil, Jefferson Luis (29), kutoka Klabu ya Resende FC ya Rio de Janeiro.

Klabu hiyo imesema imeingia mkataba wa miaka miwili na kipa huyo ambaye tayari ameungana na makipa wengine waliopo kambini nchini Uturuki, Ally Salim na Ahmed Feruzi Telu, kwa maandalizi ya mashindano ya msimu ujao, huku ikiendelea kumsubiria kipa mwingine Aishi Manula ambaye aliumia mwishoni mwa msimu uliopita na kufanyiwa operesheni itakayomweka nje zaidi ya miezi mitatu.

"Tumefanikiwa kumpata golikipa Jefferson Luis, karibu sana. Tayari mlinda mlango huyo ameungana na kikosi nchini Uturuki kuendelea na mazoezi ya maandalizi ya msimu wa mashindano 2023/24 akitokea Brazil," ilieleza taarifa ya Simba na kuongeza.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >